epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US
Jumatano Aprili 24, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581656
www.ippmedia.com
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital



UKURASA 22

**ARTETA: CHELSEA ITAFANIKIWA CHINI YA POCHETTINO**

# Mvua yazidi kuleta maafa

• **Barabara** zafungwa, wanafunzi 80,000 wakosa masomo, serikali yafikiria... *Endelea ukurasa 2*



Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda (kulia) akiteta jambo na Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge wakiwa kwenye boti alipotembelea Shule ya Msingi Mohoro, wilayani Rufiji, eneo lililoathiriwa na mafuriko. **PICHA: JULIETH MKIRERI**

UKURASA WA 4

## SAMIA AWA MBOGO UVUJAJI WA MAPATO MAMLAKA ZA MITAA, ASISITIZA UBUNIFU



RAIS Samia Suluhu Hassan amekemea vitendo vya uvujishaji mapato vinavyoendelea katika mamlaka za serikali za mitaa...

UKURASA WA 4

## BUNGE LATAKA MCHAKATO KUFUTWA MASHIRIKA MZIGO



SPIKA wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, ameitaka serikali kupitia Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji...

UKURASA WA 17

## UDHAMINI WA NMB MKUTANO MKUU ALAT WAFIKIA BIL. 1.2/-

BENKI ya NMB, imekabidhi hundi yenye thamani ya Sh. milioni 120 kudhamini Mkutano Mkuu wa 38...

## JKCI sasa yaanzisha huduma matibabu wagonjwa wa moyo nyumbani

UKURASA 3



Baadhi ya wakazi wa kata za Mwasonga na Kibada, wakiwa wameshikwa na butwaa baada ya daraja katika barabara ya Mwasonga kusombwa na maji jana na kukata mawasiliano. **PICHA: SHUKURU MANYAMA**



## TAKUKURU yakamata mawakala mbinu chafu mitandao ya kibenki

UK. 3




OFA KATIKA TOLEO MAALUM!!

Katika kuadhimisha Siku ya Muungano mwaka huu, tarehe 26 April 2024 Kampuni ya The Guardian Ltd (TGL) inayochapisha magazeti ya Nipashe na The Guardian Itatoa toleo maalum la Muungano, hivyo inawakaribisha kutoa salamu za kumbukizi, matangazo, picha na makala za mafanikio katika kusherekea miaka 60 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar kwa PUNGUZO MAALUM

Wahi mapema kwa sikukuu hii upate PUNGUZO, Artwork ya bure na nafasi katika majukwaa yetu ya kidigitali.

*vigezo na masharti kuzingatiwa*

The Guardian Nipashe

KWA MAWASILIANO TUPIGIE | +255 677 020 701

Barua pepe: advertise@guardian.co.tz Au Tutembelee The Guardian Limited, Mikocheni Light Industrial Area, Mkabala na ITV / Radio One, Dar es Salaam
Tovuti: www.ippmedia.com / epaper.ippmedia.com



Mwenyekiti wa Wazazi CCM Mkoa wa Morogoro, Dk. Rose Rwakatare (katikati) akimsikiliza Mwenyekiti wa Kitongoji cha Chikago Kata ya Minepa Wilaya ya Ulanga Morogoro, Cosmas Mazuma akielezea namna mafuriko yalivyofunika mashamba yao ya mpunga, alipotembelea eneo hilo, jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Mvua yazidi kuleta maafa maeneo mengi

**Na Waandishi Wetu**

MVUA inayoendelea kunyesha katika maeneo mbalimbali nchini, imesababisha maafa ikiwamo kuharibika kwa miundombinu, makazi ya watu kuzingirwa na maji na baadhi ya huduma kusimama.

Mitandao ya kijamii jana ilionyesha baadhi ya barabara za Dar es Salaam zikiwa zimejaa maji na kusababisha usafiri katika maeneo hayo kusimamishwa.

Aidha, baadhi ya barabara magari yalipita kwa taabu huku yale madogo yakishindwa kupita kwa sababu ya kujaa maji. Miongoni mwa maeneo hayo ni Shoppers Plaza, Mikocheni, Dar es Salaam ambako maji yalijaa barabarani.

Taarifa zaidi zilieleza kuwa mvua hiyo inayonyesha katika mikoa mbalimbali nchini, ikiwamo ya pwani, imesababisha uharibifu mkubwa wa mindombinu ikiwamo ya uchukuzi. Baadhi ya mikoa hiyo ni Pwani, Dar es Salaam, Morogoro na Arusha.

**WANAFUNZI WAKWAMA**

Zaidi ya wanafunzi 80,000 wa shule za msingi katika wilaya za Rufiji na Kibiti mkoani Pwani, wamekosa masomo kutokana na mafuriko yaliyosababishwa na mvua kubwa inayoendelea kunyesha.

Ofisa Elimu wa Mkoa wa Pwani, Sara Mlaki, aliyasema hayo jana alipokuwa kwenye ziara ya kujionea athari za mvua hizo katika shule na makazi katika wilaya za Rufiji na Kibiti ikiwamo kuharibu miundombinu ya elimu.

Ziara hiyo ilijumuisha Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolph Mkenda na Katibu Mkuu Prof. Carolyne Nombo.

Alisema shule 11 za msingi zenye wanafunzi 7264 wakiwamo wasichana 3657 na wavulana 3607 wameathirika na mafuriko wilayani Rufiji.

Aidha, alisema nyumba 58 za walimu pia zimeathiriwa na kupoteza samani na mali zilizokuwamo ndani ya nyumba hizo.

Alisema katika Wilaya ya Kibiti wanafunzi 824 katika shule saba za msingi zimeathirika huku tatu zikifungwa kutokana na adha hiyo huku sekondari ya Mtanga Delta ikiathirika pia.

"Athari za mvua ni kubwa zimeharibu miundombinu ya shule na wanafunzi kukosa sehemu za kusoma, mkoa umefanya jitihada kuhakikisha wanakuwa salama na kuainisha shule ambazo hazijaathirika na mafuriko ili zipokee wanafunzi kuendelea na masomo," alisema Sara.

Akizungumzia maafa hayo, Waziri Prof. Mkenda, alisema serikali imeweka utaratibu kwa wanafunzi wote waliokumbwa na mafuriko hayo kusoma kwenye shule maalum ambazo zimetengwa.

Mkenda alisema mwanafunzi yeyote asibaki nyumbani kwa sababu ya mafuriko na badala yake wazazi wawapeleke kwenye shule ambazo zimeainishwa na viongozi wa maeneo hayo.

Kuhusu miundombinu alisema serikali imetenga fedha kwa ajili ya kujenga mabweni, vyoo, madarasa, vifaa vya kufundishia na chakula kuwawezesha wanafunzi kusoma kwa utulivu.

Alisema tayari wizara imetoa baadhi ya vifaa vikiwamo vitabu vya kiada na ziada, madaftari na penseli na kalamu kwa wanafunzi wa shule ya sekondari Muhoro na Katundu ambazo ni miongoni mwa zinazopokea wanafunzi walioathirika na mafuriko.

Katibu Mkuu Prof. Nombo, alisema wanaendelea kufanya tathmini ya athari za mafuriko katika sekta ya elimu, lakini amepongeza jitihada za walimu kuendelea kuwapo kwenye vituo vya kazi na kufundisha licha ya mafuriko.

Akifafanua kwa wanafunzi wa madarasa yenye mitihani alisema serikali imeweka utaratibu wa kuhakikisha wote wanatambulika na kurudi shule.

Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge alisema timu ya wataalam imeweka kambi kuhakikisha wananchi wote waliokumbwa na mafuriko wanahamishiwa kwenye makambi maalum, ikiwamo ya Nyamwage ambayo imewekwa kwa ajili ya kutoa huduma zote muhimu.

• ***Grace Mwakalinga (RUFIJI) na Mwandishi Wetu, DAR***

# Serikali yafikiria kuzifunga shule

**Na Romana Mallya**

SERIKALI inafikiria kufunga shule muda wowote kuanzia sasa kutokana na athari za mvua inayoendelea kunyesha maeneo mbalimbali nchini.

Kamishna wa Elimu katika Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Lyabwene Mtahabwa (pichani), alisema jana kuwa serikali inafanya tathmini kwa kuhusisha athari ya mvua katika mikoa yote nchini kabla ya kuchukua uamuzi huo.

Akizungumza na mwandishi wa habari hii jana kwa njia ya simu kuhusu athari ya mvua inayoendelea sasa na hatua zilizochukuliwa kwa watoto shuleni, Dk. Mtahabwa, alisema: "Tulia, nimeandika barua. Hilo jambo tunalishughulikia ili tufanye tathmini mikoa yote na athari zake.



"Ikiwezekana tufunge shule kwa siku kadhaa ili watoto wawe salama. Tunalifanyia kazi, kiongozi wangu tuko makini sana. Ninashukuru sana kwa kuliona hilo, ubarikiwe," alisema.

Kuhusu lini taarifa ya kufungwa shule itatolewa, Dk. Mtahabwa alisema wakati wowote kuanzia sasa zitatolewa na hicho ndicho kipaumbele chao kwa sasa.

Wakati hatua hii ikichukuliwa, Aprili 12, mwaka huu, basi la wanafunzi katika Shule ya Mchepuo wa Kiingereza ya Ghati Memorial School ya jijini Arusha, lilitumbukia kwenye korongo lililoko eneo la Engosheratoni, Kata ya Sononi, na kusababisha vifo vya watoto saba.

Awali, Kaimu Kamanda wa Kikosi cha Usalama Barabarani nchini, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Jeshi la Polisi, Butusyo Mwambelo, akizungumza na Nipashe kuhusu athari ya mvua kwa upande wa miundombinu, alisema kwa ujumla hali ni mbaya na imesababisha baadhi ya barabara kufungwa kwa muda.

"Mfano, barabara ya Jangwani tumeifunga tangu jana (juzi) baada ya mvua kunyesha na maji kujaa. Magari yote yanaishia Magomeni na yanayotokea mjini yanaishia Fire.

"Barabara ya Nyerere, kutokana na ujenzi kuna baadhi ya maeneo yana mashimo mengi. Pia pale Vingunguti kuna ujenzi unaoendelea, shimo limejaa maji. Tunatahadharisha wananchi na wenye magari madogo na vyombo vingine vya moto wanapotumia barabara hii, wawe makini," alisema.

Kadhalika alisema eneo la Kigamboni kutokea Tungi Msikitini kuelekea katika mzunguko wa kwa Msomari kuna shimo limejaa maji.

Barabara zingine zilizoripotiwa kufungwa kutokana na maji kujaa ni Mkwajuni, Africana na ile ya kutokea Kibada kuelekea Kisarawe 2 daraja limekata mawasiliano baada ya kuvunjika.

Hadi mwishoni mwa wiki mvua hii ya masika iliathiri jumla ya wananchi 273,159 kwa wakazi wa mikoa ya Pwani, Morogoro na Mbeya na kusababisha kukosa makazi.

Alisema tayari Mkuu wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai Kanda Maalum ya Dar es Salaam (ZCO) na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, wamekwenda kufanya ukaguzi kwa sababu maji yamejaa na barabara hazipitiki. Mwambelo alisema wametoa tahadhari pia kwa wanafunzi kuwa makini hasa wanaporuhusiwa kwenda shuleni.

"Magari yanayochukua wanafunzi mengi ni madogo na yanapita barabara ambazo si za lami na mitaro mingi imeziba. Kama wanaona ni hatari ni bora shuleni wasiende kuchukua wanafunzi au wasiende shuleni kabisa ili tusisababishe maafa mengine.

"Mpaka sasa upande wa usalama barabara hatujapata maafa yoyote. Kwa upande mwingine nimewasiliana na Kamishna wa Elimu kuangalia kwa kipindi hiki kila mtu aangalie eneo lake kama kuna mvua nyingi watoto wasiende shule.

"Yaani wakafunga shule angalau siku mbili au tatu. Amepokea ombi letu na ametuambia atawasiliana na TAMISEMI (Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa) ameliona wazo hili ni zuri na ameahidi kulifanyia kazi," alisema.

Mwambelo alisema wameona shule zikifungwa kwa kuwa kuna zingine zimeshafungwa kutokana na kuathiriwa na mafuriko, watoto hawatakuwa nyuma kielimu.

**DART**

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano kwa Umma cha Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART), kuanzia jana, barabara ya Jangwani ilifungwa kutokana na mafuriko, hivyo mabasi ya njia ya Gerezani, Kivukoni yataishia Magomeni Mapipa.

Taarifa hiyo ilisema huduma ya usafiri wa DART inaendelea kutolewa kwa njia ya Morocco kwenda Kimara na maeneo ya katikati ya jiji kwa njia ya Muhimbili na Gerezani.

Pia ilisema huduma za mabasi ya mfumo wa DART zinaendelea kama kawaida kwa njia ya Kimara hadi Mbezi, Kimara hadi Kibaha na Kimara hadi Mlongazila.

## HABARI KITAIFA

# JKCI yaanzisha huduma mpya kutibu wagonjwa moyo nyumbani

**Na Romana Mallya**

TAASISI ya Jakaya Kikwete (JKCI) imeanzisha huduma mpya 'Home Based Care' kwa wagonjwa wa moyo wa nyumbani ambao watawekewa shuka maalum lenye kifaa kitakachotoa taarifa moja kwa moja hospitalini za mapigo ya moyo, umeme wa moyo na hali ya presha kwa ujumla.

Mkurugenzi Mtendaji wa JKCI, Dk. Peter Kisenge, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, akifafanua kuwa, shuka hilo maalum litakuwa na kifaa kitakachowezesha wataalam walioko JKCI kupata taarifa za mgonjwa aliyeko nyumbani moja kwa moja.

Dk. Kisenge ambaye ni Bingwa wa Magonjwa ya Moyo, alisema mgonjwa akihitaji huduma ya saa 24 akiwa nyumbani atapewa kupitia daktari au nesi.

Alisema kupitia huduma hiyo watawahudumia wagonjwa wakiwa nyumbani hususani waliokuwa wamelazwa JKCI na kuruhusiwa, lakini bado wanahitaji uangalizi maalum.

"Wakiwa nyumbani tutaendelea kuwahudumia. Tumekuja na huduma mpya kabisa ya teknolojia ya juu ambapo mgonjwa atalalia shuka maalum na kuweka kifaa maalum chini ya kitanda chake na sisi tutaweza kugundua mapigo ya moyo au umeme wa moyo na tutagundua presha zake zikoje.

"Tutaweza kujua oksijeni yake ikoje kwa kuwa wagonjwa waliozidiwa sana presha hushuka ghafla na kupoteza maisha. Akiwa nyumbani tutapata ujumbe kwamba mgonjwa yupo nyumbani na presha zimeshuka na itakuwa rahisi kumfuata aliko," alisema.

Dk. Kisenge alisema JKCI ina magari ya wagonjwa zaidi ya sita, wanaweza kumfuata mgonjwa na kumpeleka hospitalini hapo na kumhudumia.

Kupitia teknolojia hiyo mpya ambayo inatumika nchini India, wanaweza kumwambia ndugu nini cha kufanya.

"Mgonjwa anakuwa na kitanda chake tunamwekea hicho kitambaa kitakuwa kinapima mapigo ya moyo, presha na oksijeni akiwa nyumbani. Tutawahudumia wagonjwa waliozidiwa kwa kuwafuata waliko. Jamii imekuwa na watu wazima kuwaleta inakuwa shida.

"Akituambia tutamfuata aliko na kumpa huduma kwa madaktari au nesi kwenda, lakini wengine wamefanyiwa operesheni wanakuwa na vidonda wanahitaji kusafishwa, nesi wanaweza kwenda kumsafisha," alisema.

Dk. Kisenge alisema kuna wagonjwa waliokaa hospitalini kwa muda mrefu wanahitaji huduma wakiwa na ndugu zao nyumbani, hivyo JKCI itaitoa kwa madaktari au nesi kwenda kumhudumia.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Dk. Seleman Jafo akiwasilisha hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Bungeni, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# TAKUKURU yakamata mawakala mbinu chafu mitandao ya kibenki

**Na Christina Haule,** MOROGORO

TAASISI ya kuzuia na kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Mkoa wa Morogoro imewafikisha mahakamani mawakala wa huduma za kifedha wawili kwa tuhuma za kufanya mbinu chafu na kuwaibia wateja wanapofanya miamala ya kupitia akaunti zao za kibenki.

Naibu Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Morogoro, Christopher Mwakajinga, alisema hayo jana wakati akitoa taarifa ya robo tatu ya mwaka 2023/24 na kubaini mbinu hizo chafu zinazotumiwa na mawakala hao baada ya kupata taarifa kutoka wa wasiri wao na kuanza kuzifanyia kazi.

Aliwataja waliofikishwa katika mahakama ya Wilaya ya Morogoro kuwa ni Juma Msuya na Jamhuri Yohana ambao Machi 18 walifunguliwa kesi ya jinai namba 7110 ya mwaka 2024 na walikana shtaka hilo na wako nje kwa dhamana.

Mwakajina alifafanua kuwa mawakala hao wasio waadilifu wana tabia ya kupokea fedha kutoka kwa wateja wanaohitaji huduma ya kuweka fedha katika akaunti zao za benki, lakini fedha hizohaziingizwi katika akaunti walizopewa na wateja wao na badala yake wanatoa stakabadhi batili (fake) za kielektroniki ili kuwaaminisha wamewekewa fedha.

Aidha, aliishauri jamii kujenga tabia ya kuhakikisha wanapokea taarifa kupitia simu zao zinazoonesha kuwa wameingiza fedha benki na kusoma akaunti zao ili kuepusha na kukomesha mbinu hizo chafu.

"Vilevile, ninawakumbusha wananchi wanapohitaji huduma ya kuwekewa fedha katika akaunti zao za kibenki kupitia mawakala, wajiridhishe kiasi uhakiki wa fedha zao kama zimeingia katika akaunti zao kupitia ujumbe mfupi kwenye simu zao kabla ya kuondoka kwa wakala," alisema Mwakajinga.

Pia, alitoa onyo kwa mawakala wote nchini kutojaribu kufanya udanganyifu wa kujipatia fedha kinyume na matakwa ya leseni zao walizopewa na mamlaka husika kufanya biashara hiyo.

Wakati huo huo, Mwakajinga alisema TAKUKURU imefuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayohusiana na afya na elimu yenye thamani ya Sh. bilioni 9.0 ambayo ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji na kabaini miradi sita yenye thamani ya Sh. bilioni 4.5, ikiwa na upungufu na kuchukuliwa hatua mbalimbali.

Alitaja miradi hiyo kuwa ni ujenzi wa shule ya sekondari ya wasichana, Duthumi wilayani Morogoro wenye thamani ya Shilingi bilioni tatu na ufuatiliaji wa mradi wa ujenzi wa Kituo cha Afya Dakawa, wilayani Mvomero wenye thamani ya Sh. milioni 400 miradi ambayo uchunguzi wake unaendelea.

Aliitaja miradi mingine kuwa ni ujenzi wa Shule ya Sekondari Madoto, Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa wenye thamani ya Sh. milioni 500, ujenzi wa jengo la mama na mtoto mjini Ifakara wenye thamani ya Sh. milioni 500 na ujenzi wa matundu ya vyoo na sehemu ya kunawia mikono kwenye Shule ya Msingi Lilela wilayani Gairo, wenye thamani ya Sh. milioni 46.3 na ushauri mbalimbali umetolewa katika kuhakikisha ujenzi unakwenda kama ulivyopangwa

Aidha, Mwakajinga aliitaja mikakati ya TAKUKURU kwa kipindi cha Aprili hadi Juni 2024 kuwa ni kutoa elimu ya uzuiaji vitendo vya rushwa kwa wanafunzi, wananchi na watumishi wa umma na kuendeleza programu ya TAKUKURU rafiki kwa kata ambazo hazijafikiwa na kutoa mrejesho wa kata walizopitia.


**bgtl BEST GROUP (T) LIMITED**
Debts collectors, Auctioneer, Commission Agent & Legal Consultant

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA (MARUDIO)**

Kwa Idhini tuliyopewa na **C&F Law Advocate** Kwa niaba ya **BANK OF INDIA** Tutauza kwa mnada wa hadhara (marudio) dhamana ya mdaiwa wa **BANK OF INDIA** ambayo ni nyumba ya makazi kama inavyoonesha kwenye jedwali hapo chini.

| Na. | JINA LA MDAIWA | MAELEZO YA DHAMANA NA MAHALI ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|
| 1 | DAVID SIMON MZENA | Nyumba ya makazi yenye Kiwanja Na 684, kitalu" B" Kinyerezi Wilaya ya Ilala CT no.94594 iliyopo kwa jina la DAVID SIMON MZENA. | 25/04/2024 |

**MASHART YA MNADA**

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa siku ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14). Kukamilisha malipo yote. Kushindwa kufanya hivyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25%, na mnada kurudiwa, au mshindi wa pili atapewa ushindi.
4. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji na zingine zinazoambatana na hilo ni jukumu la mnunuzi.

**Kwa Taarifa zaidi wasiliana na:**
**Mkurugenzi Mtendaji**
**Best Group (T) LTD**
**Alli Hassan Mwinyi Road**
**Green Acres Buliding, 2nd Floor.**
**P.O. BOX 1088**
**DAR ES SALAAM**
**MOBILE + 255 715-363537/ +255 765-363537**

**AU**

**Mkurugenzi Mtendaji**
**C &F Law advocate,**
**3rd Floor Diamond Plaza,**
**Mirambo/Samora Ave,**
**P.O.BOX 70280**
**DAR ES SALAAM.**
**0659 734720**

**HABARI KITAIFA**

# Samia awa mbogo kuvuja mapato h/shauri, ataka ubunifu

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

RAIS Samia Suluhu Hassan amekemea vitendo vya uvujishaji mapato vinavyoendelea katika mamlaka za serikali za mitaa nchini, huku akiwatwisha mzigo mamea, wenyeviti wa halmashairi na wakurugenzi kubuni vyanzo vipya vya mapato kwenye maeneo yao.

Katika hotuba yake ya ufunguzi wa Mkutano Mkuu wa 38 wa Jumuiya ya Tawala za Mitaa Tanzania (ALAT) jana visiwani hapa, iliyosomwa kwa niaba yake na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, alisema halmashauri lazima zibuni vyanzo vipya vya mapato ili kujenga ufanisi pamoja na kuleta maendeleo ya wananchi.

"Lazima watendaji tuwe wabunifu katika halmashuri zetu. Lazima tubuni mbinu na njia ambazo tutahakikisha tunasimamia kwa asilimia kubwa katika kukusanya mapato na kwa matumizi yaliyopitishwa kwa maendeleo ya wananchi," alisema.

Pia aliwataka wakurugenzi wa halmashauri na watendaji kuwa waadilifu katika ukusanyaji wa mapato ya serikali hasa katika matumizi ya mifumo ya kisasa.

Alisema kuna taarifa za matumizi ya mashine feki ya ukusanyaji mapato jambo ambalo linaikosesha serikali mapato mengi.

"Tunazo taarifa uwepo wa mashine feki za kukusanyia mapato. Lakini pia kuna mashine ambazo taarifa za mapato haziingii lakini pia zipo mashine zinazimwa, hivyo watu hawa ambao si waadilifu watachukuliwa hatua stahiki," alisema.

Aidha aliwataka wakurugenzi wa halmashauri kusimamia vyema miradi yote inayotekelezwa katika maeneo yao ili ikamilike kwa wakati. Kwa mujibu wa Rais Samia, kuna miradi kama vile ya afya , elimu, maji na miundombimu ya barabara inayotekelezwa katika maeneo mbalimbali, hivyo haina budi kusimamiwa kwa kufika katika maeneo ya miradi hiyo.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Serikali za Mitaa na Idara Maalum ya SMZ, Masoud Ali Mohamed, alisema ALAT kwa Tanzania Bara na ZLGA kwa Zanzibar ni taasisi muhimu katika nchi na kwamba kufanikiwa kwazo ni mafanikio ya serikali.

Alisema kutofanya vizuri kwa taasisi hizo kunasababisha kufeli kwa kila sehemu ya serikali kwa kuwa serikali inaanzia ngazi za chini.

"Unaweza kuwa na sheria nzuri, posho nzuri lakini kama hakuna utashi wa kisiasa basi hatutafanikiwa, hivyo ni vyema tukawa na msingi mzuri wa utendaji kazi katika mamlaka za serikali za mitaa," alisema.

Naye Mwenyekiti wa ALAT, Murshid Ngezi, akitoa taarifa ya jumuiya hiyo, alisema kitendo cha serikali kuongeza posho kwa wakurugenzi, madiwani na watendaji wa serikali za mitaa ili kuleta ufanisi katika utendaji wa kazi zao ni cha kupongezwa.

Alisema nyongeza hiyo ya posho itasaidia watendaji hao kufanya kazi kwa ufanisi lakini pia kujitegemea katika halmashauri zao.

Pia aliipongeza serikali kwa hatua ilizochukua katika kuleta mabadiliko kwenye halmashauri na kuzifanyia kazi changamoto zilizoko.

Kadhalika, alizipongeza halmashauri zote ambazo zimefanya vizuri katika ukusanyaji wa mapato na kuziomba zingine ambazo hazijafanya vizuri, kuiga mfano wa hizo

Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Biashara Tanzania (TCB), Adam Mihayo, alisema benki hiyo itendelea kuisaidia serikali katika ngazi za chini kwenye miradi mbalimbali ya kijamii.

Alisema benki hiyo inachopata kutoka kwa wananchi, inakirejesha kupitia miradi mbalimbali ikiwamo kusaidia mikopo kwa vikundi vya ujasiriamali.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa (wa pili kushoto), akikabidhi cheti cha utambuzi na shukrani kwa Mkurugenzi wa wateja wakubwa na shughuli za serikali wa NBC, James Meitaron (wa pili kulia), kwa ajili ya kutambua mchango wa benki hiyo, kufanikisha Mkutano Mkuu wa 38 wa Mwaka wa Jumuiya ya Tawala za Mitaa Tanzania (ALAT), jijini Zanzibar jana. Wengine ni Makamu Mwenyekiti wa ALAT Taifa, Sima Costantine (kushoto) na Mkuu wa Kitengo cha Mahusiano ya Umma wa benki hiyo, Godwin Semunyu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bunge lataka mchakato kufutwa mashirika mzigo

**Na Vitus Audax,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, ameitaka serikali kupitia Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kukamilisha michakato ya kuunganisha na kufuta baadhi ya mashirika ya umma kisha kuuwasilisha bungeni kwa ajili ya kuvunjwa na kupitisha sheria mpya.

Dk. Tulia alitoa kauli hiyo juzi bungeni wakati wa kupitisha makaridirio ya mapato na matumizi ya ofisi hiyo kwa mwaka 2024/25 na kusisitiza kuwa kwa sasa serikali haitakiwi kuthibitisha kufutwa kwa mashirika hayo kwa kuwa bado sheria zilizopitishwa na bunge kuhusu kuanzishwa kwayo haijabatilishwa.

Spika alitoa kauli hiyo baada ya hoja iliyoibuliwa na Mbunge wa Kisesa (CCM), Luhaga Mpina, kuhusu wizara hiyo kutaja kufutwa kwa mashirika ya umma manne na kuunganishwa mengine 16 ilihali Bunge halikushirikishwa katika mchakato huo.

Alisema kama shirika lilianzishwa na sheria ya bunge haliwezi kufutwa kwa mchakato nje ya bunge na kutolea mfano Tume ya Mipango kuwa ilifutwa na kurejeshwa bungeni, hivyo lazima taratibu zifuatwe.

"Hoja ya Mbunge Mpina ina mantiki maana katika ule uhalisia maelezo kama ya kamati namna yalivyoandikwa hapa na ufafanuzi ulioutoa hapa na hata mimi nilipoliona tangazo niliamini kwamba mko katika kupima shirika lipi litafutwa na yapi yataunganishwa," alisema.

Aliitaka wizara hiyo pindi itakapokuwa imejiridhisha ipeleke sheria bungeni ili lifute sheria ya mashirika husika kupitia sababu zitakazowasilishwa bungeni hapo.

"Ili isilete mkanganyiko kauli ni kuwa wizara imetoa taarifa kuwa kuna hiyo nia ya kufuta kwahiyo mashirika yajieleze kama yanaona yana umuhimu au mengine yaungane na mambo kama hayo ili isionekane kama kuna utaratibu nje na utaratibu uliowekwa kisheria tulioutunga sisi wenyewe," alisema Dk. Tulia

Awali, akijibu hoja zilizoibuka bungeni, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Prof.Kitila Mkumbo, alitaja sababu za kufutwa kwa baadhi ya mashirika ya umma na mengine kuunganishwa kuwa ni pamoja na kujiendesha kwa hasara.

"Mfano mashirika yanakusanya Sh. trilioni 1.07 lakini yanatumia zaidi ya Sh. trilioni tatu, hivyo tukaona lazima yafanyiwe mabadiliko. Tuliyaunganisha 16 na kufuta manne na michakato kwa mengine bado inaendelea," alisema Prof. Mkumbo.

Aidha, alilihakikishia bunge kuwa wafanyakazi katika mashirika yanayofutwa watapangiwa maeneo mengine ya kufanya kazi kutokani na taifa kuwa na uhitaji mkubwa wa watumishi hivyo hakuna atakaye kosa kasi kwa kufutwa au kuunganishwa kwa mashirika.

**MIKAKATI KUWAINUA VIJANA**

Miongoni mwa hoja zilizoibuka katika mjadala huo ni pamoja na mkakati wa kuwashirikisha vijana katika fursa mbalimbali za mipango na uwekezaji ambao walitajwa kutengwa licha ya kuwa zaidi ya asilimia 76 ya Watanzania.

Hoja hiyo iliibuliwa na Mbunge wa Viti Maalumu (CCM), Ng'wasi Kamani, na Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA), Sophia Mwakagenda, waliotaka mikakati ya ushirikishwaji wa vijana ili kuwasaidia kukabiliana na tatizo la ukosefu wa ajira.

"Kwa sasa asilimia kubwa ya Watanzania ni vijana kwa mujibu wa Sensa ya mwaka 2022 na wizara hii imesimama kati ya masuala muhimu ya kilimo, utalii, viwanda, uchukuzi na uchimbaji madini. Sasa ni vyema mipango yake ionyeshe namna ya kuwainua vijana ili washiriki kufikia maendeleo hayo," alisema Kamani.

## Usajili laini simu wapaa Zanzibar

**Na Mwandishi wetu**

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), imesema kuwa mwelekeo wa usajili wa laini za simu za mkononi Zanzibar unaonyesha ongezeko la asilimia 12 katika upatikanaji wa huduma za simu za mkononi miongoni mwa wananchi.

Kwa mujibu wa taarifa kwa umma iliyotolewa na Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dk. Jabiri Bakari, takwimu za hali ya mawasiliano kipindi cha Januari hadi Machi, mwaka huu, zinaonyesha usajili wa laini za simu Unguja na Pemba uliongezeka kwa wastani wa asilimia 37.21 kati ya 2022 na Machi 2024.

"Serikali inatekeleza mradi mkubwa Zanzibar kuwezesha watumiaji kupata huduma bora zaidi za mawasiliano ya simu za mkononi, hasa zenye ubora kwenye maongezi na kasi ya matumizi ya data. Novemba 2022 Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilizindua ujenzi wa minara ya mawasiliano ya simu 42 katika shehia (kata) 39 Unguja na Pemba," alisema.

Alisema mradi huo ni sehemu ya mpango unaosimamiwa na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) na kwamba kwa Tanzania Bara, serikali inajenga minara 758 mipya na kuboresha mingine zaidi ya 300 na kuiongezea nguvu.

Dk. Bakari alisema takwimu za TCRA zinaonyesha kwamba kuenea kwa laini za simu miongoni mwa watu kwa Unguja na Pemba kumefikia asilimia 45 na kwamba kuenea huko kulikuwa asilimia 26.5 Septemba 2022, miezi miwili kabla ya mradi.

TANGAZO


KILIMANJARO
DRINKING WATER
A PRODUCT OF
The Coca-Cola Company
Mshindi wa
SUPERBRANDS
AFRIKA MASHARIKI
2022-2024
VOTED
Superbrands
EAST AFRICA'S CHOICE
2022-2024
Asanteni wateja wetu
Hii ni yetu sote
kilimanjaro_drinking_water
kilimanjarodrinkingwater
kdw@bbl.co.tz
+255 762628166 | +255 659785276 | +255 272754422

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wananchi msiweke rehani maisha mvua inaendelea

**MVUA** ya masika inaendelea kunyesha maeneo mbalimbali nchini na kuleta athari kubwa ya mafuriko huku wengine wakipoteza makazi na mali.

Kabla mvua hii haijaanza kunyesha Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA), ilitoa tahadhari kwa wananchi wanaoishi maeneo hatarishi kuondoka mapema ili kujiepusha na madhara.

Mabadiliko ya tabia nchi yamesababisha nchi nyingi duniani kuathirika na mvua na hata nchi zilizoendelea zenye miundombinu mizuri pia zimeathirika na mafuriko.

Katika mitandao ya kijamii kuna picha za video zinazoonesha baadhi ya nchi hizo zikipitia wakati mgumu baada ya nyumba kuzingirwa na maji huku barabara zikiwa zimejaa maji mithili ya mito.

Hii inasababishwa na mabadiliko hayo ni hali ambayo haiwezi kunyoosheana vidole.

Hatahivyo, athari hizo zimekuwa zikijadiliwa kote duniani na cha muhimu ni kuendelea kuchukua tahadhari ili binadamu na mali zao zisiendelee kuangamia.

Kuna nchi ambazo maisha ya watu yamepotea kwa kusombwa na maji na vile vile, mali ikiwamo magari yakisombwa na mafuriko hayo.

Kwa nchi zinazoendelea kama Tanzania, athari hizo zinaweza kuepukika kama wanaoishi kwenye maeneo hatarishi wataondoka na kutafuta sehemu nyingine zenye usalama zaidi.

Kuna umuhimu pia wa kuimarisha miundombinu ya barabara ikiwamo mitaro inayopitisha maji kutunzwa ili uchafu usitupwe ndani kuruhusu maji yanapokuwa mengi kupita bila tatizo.

Hata hivyo, kumejitokeza tabia kwa baadhi ya watu kuendelea kuharibu miundombinu hiyo kwa kutupa taka na kusababisha maji kushindwa kupita na kwenda baharini.

Hili la utupaji taka kwenye mitaro linasababishwa pia na kutozingatia usafi wa mazingira hasa uzoaji taka kwenye mitaa na maeneo ya watu wanaofanyia biashara hasa pembezoni mwa barabara.

Mitaani nyumba nyingi zimejitahidi kukusanya taka na kuzihifadhi kwenye mifuko, lakini magari ya kusomba taka hizo hayajaonekana kwa muda mrefu na matokeo yake taka hizo zinajaa na kuanza kuchafua mazingira.

Kuna wananchi ambao wanaishi kwenye mazingira hatarishi ambayo kila mvua inaponyesha nyumba zao zinazingirwa na mafuriko, lakini wako radhi kuishi kwenye adha hiyo kwa madai kuwa mvua itapita na maisha yataendelea kama kawaida.

Wengine wanagoma kuondoka kwenye maeneo hayo hatarishi wakidai kuwa ni karibu na mjini ambako sehemu za shughuli za kujipatia kipato zinafikika bila kuhitaji kutumia nauli kupanda usafiri wa umma.

Watu hao hao, huwa wa kwanza kulalamika pale mafuriko yanapoharibu nyumba na mali zao na kuilaumu serikali kuwa haiwajali.

Baadhi ya watu wameamua kuweka rehani maisha yao kwa kuamini kuwa mvua itanyesha mara moja na kuondoka zake, mpaka itakaponyesha wakati mwingine wao watakuwa wamerudi kwenye maisha yao ya kawaida.


Kwa mujibu wa TMA mvua hii ya masika itanyesha katika mikoa mingi nchini na wananchi wametakiwa kuchukua tahadhari ya hali ya juu ili wasiweze kudhurika.

Maeneo yaliyoanza kuathiriwa na mvua hiyo yameonekana ikiwamo Rufiji ambako nyumba nyingi zimefunikwa na maji na watu kufa maji baada ya kusombwa na mafuriko.

Tumaini la kupata mavuno limeondoka baada ya mazao yao kusombwa na kinachohitajika ni msaada kunusuru ndugu zetu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita. 0713 578284,
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com



Muungwana Lazima Nilonge

# Tukifanya haya maafa yatapungua

Na Joyce Lameck

**ATHARI** ya mvua inayoendelea maeneo mbalimbali ya nchi hata na nje ya mipaka, inatosha kuwa sababu ya kuchukua tahadhari baada ya kushuhudia Mlima Kawetere mkoani Mbeya ukiporomoka na ardhi kumomonyoka kwenye matukio yanayotokea mkoani Shinyanga.

Si hivyo, hata mkoani Pwani na Morogoro hali si salama maelfu ya wakazi wa maeneo hayo wameathiriwa na mafuriko na kusababisha adha kubwa hasa baada ya nyumba, vitega uchumi na mazao mashambani kufunikwa na maji.

Mbali na athari hizo ni ukweli kuwa mvua ni muhimu kwa kilimo, ufugaji, mazingira na upatikanaji wa maji kwenye mito, maziwa na vyanzo vingine kuanzia chemichemi, ndani ya ardhi oevu na misitu ya lindimaji.

Athari za mafuriko ni kubwa hivyo jamii isisahau kuwa kinga ni ya kwanza kuliko tiba na kuchukua tahadhari ikiwemo kujenga mbali na vyanzo vya maji, kuondoka mabondeni , karibu na mabwawa na maziwa pia kuacha kuziba au kuzuia mikondo ya maji na kuchafua mito na maziwa.

Walioko mabondeni la muhimu ni kuhama, kwani kuendelea kubaki ni kujiweka hatarini kusombwa na maji mvua zinapoongezeka.

Kwa mujibu wa Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA) Dk. Ladislous Chang'a, msimu huu wa masika una vipindi vya mvua kubwa zinazoweza kujitokeza na kusababisha mafuriko na maporomoko ya ardhi ambayo yameshuhudiwa.

Ni angalizo analotoa Februari mwaka huu kwa waandishi wa habari wakati akitangaza utabiri wa mvua za masika mwaka huu.

Ikumbukwe msimu wa masika unaleta mvua kwa karibu Tanzania nzima TMA, ikisema mvua hizo zilitarajiwa kuongezeka, hivyo ni suala linalohusu nchi nzima.

Kutokana na kuwa na matarajio ya uwepo wa mvua hizo kubwa kutakuwa na vipindi vya unyevu wa kuzidi kiasi pamoja na mafuriko, yote hayo yanaweza kujitokeza na kuathiri ukuaji wa mazao.

Katika utabiri huo, TMA ilieleza kuwa kuna uwezekano wa maji kujaa na kuongezeka zaidi na kuutaka umma kufahamu kuwa athari nyingine zinazotarajiwa kutokea ni ni kuongezeka kwa kina cha maji katika mito na mabwawa, maziwani na magonjwa ya mlipuko yanaweza kujitokeza kutokana na uchafuzi wa maji.

Ni wazi kwamba serikali na viongozi wanahamasisha kuhusu watu wanaojenga kwenye mabonde na mikondo ya maji kuondoka maeneo hayo na kwa ujumla kuchukua tahadhari.

Kwa ujumla huu siyo wakati wa kupuuza tena maana Watanzania wanaweza kuona kuwa hilo ni jambo la kawaida. Ni vema kujihadhari ili kuwa salama na kufurahia matunda ya mvua.

Kuna mambo ambayo yanahitaji kupewa msisitizo mathalani, serikali iweke mkazo zaidi katika kampeni za kuzuia kujenga nyumba pia ibomoe nyumba mabondeni.

Kama ambavyo Wakala wa Taifa wa Barabara (TANROADS), anavyodhibiti kujenga kando ya barabara kadhalika nyumba hizo zifuatiliwe na kuondolewa badala ya kungoja zilete maafa.

Ni wakati wa kuweka mipaka au vigingi kwenye mito na maziwa na hata mabwawa kazi hiyo ipo mipaka na alama zinazozuia au kuitenganisha jamii na misitu ya asili, mapori tengefu na mbuga za wanyama.

Ziwekwe alama hizo na kudhibiti uvamizi na ujenzi holela kwenye mabonde ya mito na maziwa na hata mabwawa kazi hiyo ikifanywa kwa ushirikiano na wizara mbalimbali kama Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira.

Aidha, Baraza la Taifa la Uhifadhi wa Mzingira, Wakala wa Huduma za Misitu, wIzara za Maji, Maliasili na Utalii, Kilimo, Uvuvi na Ufugaji, Ardhi na Makazi na pia mamlaka za maji na mazingira za mikoa na mijina mashirika ya kuendeleza mabonde wote wahusike.

Wakati mwingine kuishi katika mazingira yasiyokuwa na sheria za kudhibiti kunaweza kuwa chanzo cha uvamizi wa vyanzo vya maji na kujenga mabondeni na kwenye mabwawa.

Zitungwe sheria ndogo ndogo wilayani au halmashauri zenye hukumu na faini kuwadhibiti watakaobainika kukiuka taratibu, maelekezo na sheria zinazozuia kuzuia shughuli za kibinadamu kwenye maeneo hayo.

## HABARI KITAIFA

## Bashungwa ataka apatiwe majina mameneja wazembe

**Na Gwamaka Alipipi**

WAZIRI wa Ujenzi, Innocent Bashungwa amemuagiza Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA), Lazaro Kilahala, kumpatia majina ya mameneja wa kanda na mikoa wa TEMESA ambao wameshindwa kuwahudumia wananchi.

Alitoa agizo hilo juzi jijini Dodoma baada ya kupokea malalamiko ya mara kwa mara kuhusu huduma zinazotolewa na TEMESA ikiwamo huduma ya kivuko cha Mv. Tanga, kuwa alimuagiza Katibu Mkuu kuingilia kati kubaini changamoto zinazokwamisha kivuko hicho.

"Mambo mengi ya kiutendaji yanaletwa kwa waziri na Katibu Mkuu wakati watendaji mpo na tumewaamini kusimamia taasisi zenu, hasa jambo hili lipo TEMESA. Mtendaji Mkuu kama kuna upungufu wa wasaidizi wako bora uje kwa Katibu Mkuu useme huyu hatufahi aondoke kuliko kukaa nao, maana hatimaye jumba bovu litakuangukia wewe," alisema Bashungwa.

Pamoja na mambo mengine, Bashungwa alimtaka Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Balozi Aisha Amour, kuangalia namna bora ya usimamizi wa TEMESA katika huduma ya vivuko nchini ili kuleta manufaa na uboreshaji wa huduma za usafiri na usafirishaji ziimarike.

Aidha, alisema TEMESA inaendelea na majukwamo na kutotekeleza majukumu yake kwa uharaka pindi tatizo linapogundulika katika vivuko na hivyo kusababisha kuzorota kwa huduma hiyo katika baadhi ya maeneo.

"Changamoto ya marekebisho ya kivuko cha Mv. Tanga yanaendelea zaidi ya siku 10 sasa, lakini leo naulizia vifaa bado havijafika, kama 'parts' ziko Dar es Salaam inachukua saa ngapi hadi kufika Tanga? Na sio Tanga pekee ni maeneo yenye vivuko."

# ACT Wazalendo yataka tathmini mafuriko Rufiji

**Na Elizabeth Zaya,** RUFIJI

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimeitaka serikali kufanya tathmini ya kina ya athari za mafuriko kwa wananchi wilayani Rufiji, mkoani Pwani na kutafuta suluhisho la haraka.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Kiongozi wa chama hicho, Doroth Semu, wakati akizungumza na Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, katika ziara yake na ujumbe wake ya kutoa mkono wa pole kwa waathirika wa mafuriko Rufiji.

Alisema lililowatokea wananchi hao ni kubwa kutokana na athari hizo, hivyo kufanyika tathmini hiyo ya athari itajibu maswali yote ambayo wanaulizwa kuhusu mafuriko hayo na kutafuta ufumbuzi wa kudumu.

"Kwa hiyo sisi kama chama cha siasa ambacho pamoja na mambo mengine tuko kwa ajili ya wananchi, tutafurahi sana endapo hili la tathmini ya kina litafanyika na waathirika wakasaidika," alisema Doroth.

Doroth alisema chama kikiwa kinaadhimisha miaka 10 tangu kuanzishwa, kimeamua kutembelea waathirika hao wa mafuriko wilayani Rufiji.

Alisema miongoni mwa misaada waliyoitoa ni vyakula, nguo, sabuni, mafuta ya kula, vyombo na kwamba jumla ni tani tatu na thamani ya Sh. milioni 6.5.

Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakari Kunenge, alisema kwa tathmini ya awali ya athari za mafuriko kwenye mkoa huo mpaka sasa vifo ni watu tisa.

"Na vifo hivi sio vimetokea kwenye nyumba zilizozingirwa hapana, vyote vimetokea wakati watu wakivuka na mitumbwi," alisema Kunenge.

Alisema mpaka sasa wamepiga marufuku wananchi kutumia usafiri wa mitumbwi na badala yake usafiri unaotumika kwa sasa ni boti ambazo zimepelekwa na wadau mbalimbali.

Kadhalika, alisema tathmini ya kina kwa ajili ya athari hizo za mafuriko inaendelea kufanywa.

Mkuu wa Wilaya ya Rufiji, Meja Edward Gowele, alisema kwa wilaya, vifo vilivyotokana na mafuriko hayo ni saba ambavyo vyote vimetokea wakati wa kuvuka kwa mitumbwi.

Meja Gowele, alisema mpaka sasa kata 12 kati ya 13 zimeathirika na mafuriko hayo wilayani Rufiji.

Alisema zaidi watu elfu 89,000 wameathirika na mafuriko hayo, kaya zikiwa ni 23,360 zilizozingirwa na maji na nyumba zilizoathirika ni 628.

"Lakini tunawashukuru Rais Samia Suluhu Hassan, ametuletea chakula cha kutosha, wadau mbalimbali na kwakweli wamejitahidi kutuletea misaada ya chakula na kinagawiwa kwa waathirika wote, tunashukuru sana," alisema Meja Gowele.


## NOTISI/TANGAZO

**LEGENDS AUCTION MART LTD, DESTENI COMPANY LIMITED, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,HEDANE ENTERPRISES LTD, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS, JY AUCTIONEERS CO.LTD,DRM AUCTIONEERS & CO.LTD, MAS AND ASSOCIATES CO.LTD,MELVA INTERNATIONAL LTD ,SUMA JKT AUCTION MART COMPANY LTD,MAJEMBE AUCTION MART LTD, MABUNDA AUCTIONEER MART CO.LTD, TRUST RECOVERIES LTD, BEST GROUP (T) LTD,JAMOK INVESTMENT LTD,MCHINGA AUCTION MART,GADAU AUCTION MART,AMI AUCTION MART, IGALULA AUCTION MART,BAHARI AUCTION MART, ADILI AUCTION MART,KOTI BROTHERS CO. LTD,PROPERTY MASTER LTD,MULTLINK AGENCY LTD,TWINS AUCTIONS MART, BID CITY AUCTION,JALAS AUCTION MART,HOLLYNESS COMPANY LTD** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya AKIBA COMMERCIAL BANK PLC, tunatoa notisi ya kulipa deni kwa mdaiwa, Vinginevyo, tutafanya Minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| ARUSHA | EMMANUEL LEJASA KIMATH | NYUMBA | EMMANUEL LEJASA KIMATI | SINONI -ARUSHA | 08/05/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | MASANJA JAMES WANNA | KIWANJA | MASANJA JAMES WANNA | TERRAT - ARUSHA | 27/04/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| ARUSHA | BERTHA JEREMIA MBISE | NYUMBA | JOHN ELIPOKEA PALLANGYO | NKOARANGA | 10/05/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | HEALSUN PRE & PRIMARY SCHOOL | NYUMBA | LILIAN PHILEMON LAIZER &EDWARD N. LAIZER | SEKEI-ARUSHA | 09/05/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | FRANK RUBEN AKYOO | NYUMBA | FRANK RUBEN AKYOO | NKOARISAMBU-ARUMERU | 15/05/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | RABSON NICHOLOUS SWAI | NYUMBA | RABSON N. SWAI | LEGURUKI-MERU | 10/05/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | JACQUILINE REGINALD MARANDU | NYUMBA | ERNEST NGOWI | MURIET- ARUSHA | 08/05/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | OLIVER STANLEY MNDEME | NYUMBA | OLIVER STANLEY MNDEME | KIMANDOLU-ARUSHA | 09/05/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | DISMAS JEROME MALLYA | NYUMBA | EMMANUEL NAFTALI NGUVILA | SOKONI I -ARUSHA | 14/05/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | LABANI SAMSONI MAKALA | NYUMBA | LABANI SAMSONI MAKALA | SINONI- ARUSHA | 14/05/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | ALLEN MARTIN ISSANGYA | NYUMBA | ALLEN MARTIN ISSANGYA | AMBURENI-ARUSHA | 15/05/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | ERASTO STEPHANO LUKUMAY | NYUMBA | ERASTO STEPHANO LUKUMAY | SASI- ARUSHA | 16/05/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| AGGREY | INNOCENT DIDAS MUMBURI | NYUMBA | KHADIJA SEIF SINKAMBA | VINGUNGUTI- ILALA | 27/04/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| AGGREY | RAJABU MOHAMED MUOMBWA | NYUMBA | RAJABU MOHAMED MUOMBWA | YANGEYANGE-MSONGOLA | 29/04/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA (MARUDIO) |
| DODOMA | CHARLES SIMON MALOMELE | NYUMBA ( 2) | CHARLES SIMON MALOMELE | NDACHI-DODOMA | 08/05/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | MERY STANLEY MOSHA | NYUMBA | MERY STANLEY MOSHA | LUGURUNI-UBUNGO | 30/04/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UKONGA | NASSOR KHALID OTHMAN | NYUMBA | BAHATI SUMBU MTINDYA | MBEZI MAKABE | 29/04/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEGETA | SADICK HASSAN NDEGE | NYUMBA | SADICK HASSAN NDEGE | NYAKASANGWE-TEGETA | 08/05/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | PILI RAMADHANI MWINJUMA | NYUMBA | AMANI GREYSON MSELE | MZINGA KITUNDA | 09/05/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | MOHAMED SHABAN CHAKUSAGA | NYUMBA | MOHAMED SHABAN CHAKUSAGA | ULONGONI 'A' GONGOLAMBOTO | 09/05/2024 SAA 6:00 MCHANA NA KUENDELEA |
| UKONGA | LULU IBRAHIM SWAI | NYUMBA | MUSTAFA HASSAN NYAKIRARIA | KISIWANI BONYOKWA | 10/05/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | JAMES BENEDICT NGUSI | NYUMBA | JAMES BENEDICT NGUSI | YANGEYANGE MSONGOLA | 14/05/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | MAGABE RYOBA ISYANGA | NYUMBA | MAGABE RYOBA ISYANGA | RADA MAJOHE | 14/05/2024 SAA 6:00 MCHANA NA KUENDELEA |
| UKONGA | LAMECK RICHARD RWEYONGEZA | NYUMBA | LAMECK RICHARD RWEYONGEZA | KIVULE | 30/04/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UKONGA | MASUDI JUMANNE RAMADHANI | NYUMBA | BEATRICE STEPHANO KISHERU | SARANGA | 13/05/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBAGALA | SULTAN MSHINDO KATUNDU | NYUMBA | SULTANI M.KATUNDU | KIMANZICHANA | 08/05/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | BRILUCK SECRETARIAL SERVICE | NYUMBA | ADOLF ANSELM MNG'ANYA | KWEMBE MSAKUZI | 08/05/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | SUMAIYA ABDALLAH OMARY | NYUMBA (2) | SUMAIYA ABDALLAH OMARY | 1. KIMARA SARANGA 2.KIMARA GOLANI | 09/05/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | FRANK SAID SALUM | NYUMBA | FRANK SAID SALUM | KIVULE | 10/05/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | KIGODA ABBASI KIGODA | NYUMBA | KIGODA ABBASI KIGODA | VIGWAZA | 29/04/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |

**MASHARTI YA MNADA**

1 Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Nyumba, Kiwanja, Gari au Shamba ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2 Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali,hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.
3 Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no.0754376493/0715363537/0715868000/0714939933/0785242219/0759282344/0787129539/0767808848/0754497396/0678799566/0655715138/0759648448
4 Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba Benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi Benki bila gharama yeyote.

Access Microfinance Bank Tanzania

# ACCESS MICROFINANCE BANK TANZANIA LIMITED

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA ZISIZOKAGULIWA KWA UMMA

### IMETOLEWA CHINI YA KANUNI YA 7 NA YA 8 YA KANUNI ZA MABENKI NA TAASISI ZA FEDHA (UONESHAJI) YA MWAKA 2014

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31 MACHI 2024

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya sasa 31 MACHI 2024 | Robo Mwaka iliopita 31 DISEMBA 2023 |
|---|---|---|---|
| A. | MALI | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 6,191 | 8,403 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 7,017 | 6,516 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | - | - |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 221 | 147 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 13 | 17 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 200 | 204 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 59,216 | 55,240 |
| 12 | Mali Nyingine | 4,803 | 4,623 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 3,189 | 3,428 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **80,850** | **78,578** |
| B. | DHIMA | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | - | 501 |
| 18 | Amana za Wateja | 64,068 | 61,735 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 889 | 1,055 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 1,569 | 1,408 |
| 27 | Dhima Nyingine | 5,381 | 5,251 |
| 28 | Madeni | - | - |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **71,907** | **69,950** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI *(16 kutoa 29)*** | **8,943** | **8,629** |
| C. | FEDHA ZA WANAHISA | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 40,000 | 40,000 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | - | - |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | (31,371) | (32,537) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 314 | 1,166 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | - | - |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **8,943** | **8,629** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 235 | 653 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 3,573 | 3,780 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 4,514 | 4,761 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | 64 | 64 |
| D. | BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 11.06% | 10.98% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 5.61% | 6.31% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 99.47% | 96.41% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 73.24% | 70.30% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 73.49% | 70.56% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 2.94% | 4.32% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 2.89% | 1.72% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 MACHI 2024

(Amounts in million shillings)

| | Robo ya Mwaka sasa 31 MACHI 2024 | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31 MACHI 2023 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31 MACHI 2024 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31 MACHI 2023 |
|---|---|---|---|---|
| 1 Mapato ya Riba | 6,677 | 5,872 | 6,677 | 5,872 |
| 2 Gharama za Riba | (1,174) | (1,200) | (1,174) | (1,200) |
| 3 Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2) | 5,503 | 4,672 | 5,503 | 4,672 |
| 4 Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (356) | (465) | (356) | (465) |
| **6 Mapato Yasiyo ya Riba:** | **1,191** | **1,267** | **1,191** | **1,267** |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | (46) | 25 | (46) | 25 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 386 | 351 | 386 | 351 |
| 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| 6.4 Mapato Mengine | 850 | 891 | 850 | 891 |
| **7 Gharama Zisizo za Riba:** | **(5,921)** | **(4,898)** | **(5,921)** | **(4,898)** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | (3,306) | (3,147) | (3,306) | (3,147) |
| 7.2 Ada na Kamisheni | (156) | (130) | (156) | (130) |
| 7.3 Gharama Nyingine | (2,460) | (1,621) | (2,460) | (1,621) |
| **8 Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **417** | **576** | **417** | **576** |
| 9 Tengo la Kodi ya Mapato | (103) | (172) | (103) | (172) |
| **10 Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **314** | **404** | **314** | **404** |
| 11 Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha) | - | - | - | - |
| **12 Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **314** | **404** | **314** | **404** |
| 13 Idadi ya Waajiriwa | 376 | 392 | 376 | 392 |
| 14 Mapato kwa Hisa | 31 | 40 | 31 | 40 |
| 15 Idadi ya Matawi | 8 | 8 | 8 | 8 |
| BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI | | | | |
| (i) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 1.56% | 2.23% | 1.56% | 2.23% |
| (ii) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 14.23% | 20.77% | 14.23% | 20.77% |
| (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 75.25% | 68.61% | 75.25% | 68.61% |
| (iv) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 37.89% | 37.93% | 37.89% | 37.93% |

### BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA ILIYOISHIA 31 MACHI 2024

**Katika kuanda taarifa za hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilizile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita.**

| Jina | Cheo | Sahihi | Tarehe |
|---|---|---|---|
| Julius Justine Ruwaichi | Afisa Mtendaji Mkuu | Imesainiwa | 22 Aprili 2024 |
| Tajinder Singh Bhachu | Mkuu wa Fedha | Imesainiwa | 22 Aprili 2024 |
| Beatrice Temba | Kaimu Mkaguzi Mkuu wa Ndani | Imesainiwa | 22 Aprili 2024 |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.

| Jina | Cheo | Sahihi | Tarehe |
|---|---|---|---|
| Thomas Engelhardt | Mwenyekiti | Imesainiwa | 22 Aprili 2024 |
| Johannes Mainhardt | Mkurugenzi | Imesainiwa | 22 Aprili 2024 |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 MACHI 2024

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | (Kiasi kwa shilingi milioni) | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Robo Mwaka ya sasa 31 MACHI 2024 | Robo Mwaka iliyopita 31 DISEMBA 2023 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31 MACHI 2024 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31 MACHI 2023 |
| **I: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | 417 | 99 | 417 | 572 |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | | | | |
| - Hasara Katika Mali | 409 | 338 | 409 | 894 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (3,976) | (1,295) | (3,976) | (3,352) |
| - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | (8) | (19) | (8) | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 1,833 | 2,588 | 1,833 | 1,686 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 479 | (968) | 479 | 137 |
| -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (261) | (176) | (261) | (366) |
| - Kodi Iliyolipwa | (63) | (55) | (63) | (75) |
| - Mengineyo (bainisha) | (279) | (88) | (279) | (58) |
| *Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji* | **(1,449)** | **424** | **(1,449)** | **(563)** |
| **II: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | (129) | (43) | (129) | (43) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | 8 | 19 | 8 | - |
| Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| Mapato ahirishwa | (31) | (47) | (31) | (17) |
| *Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji* | **(152)** | **(71)** | **(152)** | **(60)** |
| **III: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| Mengineyo (bainisha) | (324) | (143) | (324) | (225) |
| Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha | **(324)** | **(143)** | **(324)** | **(225)** |
| | | | - | - |
| **IV: Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | **(1,925)** | **210** | **(1,925)** | **(848)** |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Kipindi | **11,744** | **11,534** | **11,744** | **10,277** |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Kipindi | **9,819** | **11,744** | **9,819** | **9,429** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31 MACHI 2024

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | (Kiasi kwa shilingi milioni) | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Jumla |
| **Kipindi cha sasa hadi 31 Machi 2024** | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka 2024 | 40,000 | - | (31,371) | - | - | 8,629 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 314 | - | - | 314 |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa 31 Machi 2024** | **40,000** | **-** | **(31,057)** | **-** | **-** | **8,943** |
| **Kipindi cha Mwaka uliopita hadi 31 Disemba 2023** | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka 2023 | 40,000 | - | (32,537) | - | - | 7,463 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 1,166 | - | - | 1,166 |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa 31 Disemba 2023** | **40,000** | **-** | **(31,371)** | **-** | **-** | **8,629** |




## TANGAZO


Access Microfinance Bank Tanzania

### ACCESS MICROFINANCE BANK TANZANIA LIMITED

# MINIMUM DISCLOSURES OF BANK CHARGES AND FEES

| DESCRIPTION | CHARGE/FEE | |
|---|---|---|
| **ACCESS RAHISI,NORMAL SAVINGS, RAHISI CAA, ELIMU, AND KIKUNDI ACCOUNT(RAHISI ACCOUNT)** | **TZS** | **USD** |
| Required minimum opening balance | 10,000.00 | - |
| Monthly service fees | 2,000.00 | - |
| Cash withdrawal over counter up to 10M | 3,000.00 | - |
| Cash withdrawal over counter >10M | 10,000 | - |
| Bank statement 1free per month | FREE | - |
| Bank statement subsequent months | 10,000.00 | - |
| New ATM card issuance | 10,000.00 | - |
| ATM card renewal or replacement | 10,000.00 | - |
| Replacement of the PIN | 10,000.00 | - |
| Standing order Internal | 2,000.00 | - |
| Standing order External | 12,980.00 | - |
| Dormant account fee | FREE | - |
| Interbank Transfer | | - |
| 0-10,000,000 | 2,000.00 | - |
| 10,000,001-50,000,000 | 5,000.00 | - |
| >50,000,000 | 10,000.00 | - |
| International transfer | | Up to USD 55 |
| Closure of account | 10,000.00 | - |
| **NUFAIKA TRANSACTIONAL ACCOUNT** | | |
| Required minimum opening balance | 50,000.00 | 25.00 |
| Monthly service fees | 6,000.00 | 3.00 |
| Bank statement 1free per month | FREE | FREE |
| Bank statement subsequent months | 10,000.00 | 10.00 |
| New ATM card issuance | 15,000.00 | N/A |
| Fees per ATM withdrawal | 2,000.00 | N/A |
| Interbank transfer | | |
| 0-10,000,000 | 2,000.00 | 1.00 |
| 10,000,001-50,000,000 | 5,000.00 | 2.10 |
| >50,000,000 | 10,000.00 | 4.20 |
| International transfer | N/A | Up to USD 55 |
| ATM mini statement | 1,000.00 | N/A |
| Standing order Internal | 2,000.00 | 1.00 |
| Standing order External | 12,980.00 | 12.98 |
| Dormant account fee | FREE | FREE |
| Reactivation of Dormant account | FREE | FREE |
| Letter of recommendation and certificate of balance | 50,000.00 | 23.00 |
| **NORMAL CURRENT ACCOUNT (NUFAIKA ACCOUNTS)** | **TZS** | **USD/EURO** |
| Required minimum opening balance | 100,000.00 | 50.00 |
| Monthly service fees | 6,000.00 | 3.00 |
| Cash withdrawal over counter up to 10M | 3,000.00 | 0.18% |
| Cash withdrawal over counter >10M | 10,000 | 10 |
| Fees per ATM withdrawal | 2,000.00 | N/A |
| ATM mini statement | 1,000.00 | N/A |
| Bank statement once free per month | FREE | FREE |
| Bank statement subsequent months | 10,000.00 | 10.00 |
| Cheque book 25 leaves | 20,000.00 | 10.00 |
| Cheque book 50 leaves | 35,000.00 | 15.00 |
| Dishonored cheque | 30,000.00 | 30.00 |
| Bankers Cheque | 50,000.00 | N/A |
| Stop payment | 30,000.00 | 30.00 |
| Standing order Internal | 2,000.00 | 1.00 |
| Standing order External | 12,980.00 | 12.98 |
| Balance enquiry | 1,000.00 | 1.00 |
| New ATM card issuance | 15,000.00 | N/A |
| ATM card renewal or replacement | 15,000.00 | N/A |
| Interbank transfer | | |
| 0-10,000,000 | 2,000.00 | 1.00 |
| 10,000,001-50,000,000 | 5,000.00 | 2.10 |
| >50,000,000 | 10,000.00 | 4.20 |
| International transfer | $ 55 | 55.00 |
| Dormant account fee | FREE | FREE |
| Reactivation of Dormant account | FREE | FREE |
| Letter of recommendation and certificate of balance | 50,000.00 | 23.00 |
| **SPECIAL ACCESS NUFAIKA ACCOUNT** | **TZS** | **USD/EURO** |
| Required minimum opening balance | 100,000.00 | 50.00 |
| Monthly service fees | 60,000.00 | 50.00 |
| Minimum monthly turover | 20,000,000.00 | 10,000.00 |
| Cash withdrawal over counter | FREE | 0.18% |
| Fees per ATM withdrawal | 2,000.00 | N/A |
| ATM mini statement | 1,000.00 | N/A |
| Bank statement once free per month | FREE | FREE |
| Bank statement subsequent months | 10,000.00 | 10.00 |
| Cheque book 25 leaves | 20,000.00 | 10.00 |
| Cheque book 50 leaves | 35,000.00 | 15.00 |
| Dishonored cheque | 30,000.00 | 30.00 |
| Bankers Cheque | 50,000.00 | N/A |
| Stop payment | 30,000.00 | 30.00 |
| Standing order Internal | 2,000.00 | 1.00 |
| Standing order External | 12,980.00 | 12.98 |
| Balance enquiry | 1,000.00 | 1.00 |
| New ATM card issuance | 15,000.00 | N/A |
| ATM card renewal or replacement | 15,000.00 | N/A |
| Interbank transfer | | |
| 0-10,000,000 | 2,000.00 | 1.00 |
| 10,000,001-50,000,000 | 5,000.00 | 2.10 |
| >50,000,000 | 10,000.00 | 4.20 |
| International transfer | N/A | 55.00 |
| Dormant account fee | 5,000.00 | 5.00 |
| Reactivation of Dormant account | FREE | FREE |
| Letter of recommendation and certificate of balance | 50,000.00 | 23.00 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **MIKAKATI SAVING ACCOUNTS** | | | **TZS** | **USD/EURO** | |
| Required minimum opening balance | | | 20,000.00 | 20.00 | |
| Monthly service fees | | | FREE | FREE | |
| Bank statement 1free per month | | | FREE | FREE | |
| Bank statement subsequent months | | | 10,000.00 | 10.00 | |
| Cash withdrawal over counter | | | 1 FREE WITHDRAW PER MONTH | 1 FREE WITHDRAW PER MONTH | |
| Subsequent Cash withdrawal over counter | | | 20,000.00 | 20.00 | |
| Dormant account fee | | | FREE | FREE | |
| International transfer | | | N/A | Up to USD 55 | |
| Account closure | | | 12,000.00 | 5.00 | |
| **MIKAKATI PLUS SAVING ACCOUNTS** | | | **TZS** | **USD/EURO** | |
| Required minimum opening balance | | | 10,000.00 | | |
| Monthly service fees | | | FREE | | |
| Bank statement once free per month | | | FREE | | |
| Bank statement subsequent months | | | 10,000.00 | | |
| Cash withdrawal over counter | | | ONCE FREE PER MONTH | | |
| Subsequent Cash withdrawal over counter | | | 5,000.00 | | |
| Dormant account fee | | | FREE | | |
| International transfer | | | N/A | Up to USD 55 | |
| Account closure | | | 12,000.00 | | |
| **KIKUNDI SAVING ACCOUNT** | | | **TZS** | | |
| Required minimum opening balance | | | 10,000.00 | | |
| Monthly service fees | | | FREE | | |
| Bank statement once free per month | | | FREE | | |
| Bank statement subsequent months | | | 10,000.00 | | |
| Cash withdrawal over counter | | | 3,000.00 | | |
| Subsequent Cash withdrawal over counter | | | 3,000 | | |
| Dormant account fee | | | FREE | | |
| International transfer | | | N/A | Up to USD 55 | |
| Account closure | | | FREE | | |
| **BARAKA JUNIOR ACCOUNT** | | | **TZS** | **USD/EURO** | |
| Required minimum opening balance | | | - | - | |
| monthly service fees | | | FREE | FREE | |
| Bank statement 1free per month | | | FREE | FREE | |
| Bank statement subsequent months | | | 10,000.00 | 10.00 | |
| Cash withdrawal over counter | | | FREE | FREE | |
| Subsequent Cash withdrawal over counter | | | FREE | FREE | |
| Dormant account fee | | | FREE | FREE | |
| International transfer | | | N/A | Up to USD 55 | |
| Account closure | | | FREE | FREE | |
| **TERM DEPOSIT RATES 2023** | | | | | |
| **Amount** | | | **Interest Rates** | | |
| 5,000,000 - 500,000,000 | | | 3% - 12% p.a | | |
| > 500,000,000 | | | Negotiation | | |
| **AGENCY BANKING** | **To Govt** | **Old Customer Fee** | **To AMBT** | **To Agent** | **New Customer Fee** |
| **Withdrawal (TZS) (agents) Range** | | | **TZS** | | |
| 100-2999 | 10 | 710 | 450 | 350 | 810 |
| 3000-3999 | 14 | 711 | 450 | 350 | 814 |
| 4000-4999 | 27 | 719 | 450 | 350 | 827 |
| 5000-6999 | 54 | 739 | 450 | 350 | 854 |
| 7000-9999 | 56 | 770 | 450 | 350 | 856 |
| 10000-14999 | 102 | 788 | 450 | 350 | 902 |
| 15000-19999 | 195 | 924 | 450 | 350 | 995 |
| 20000-20000 | 306 | 1,127 | 450 | 350 | 1,106 |
| 20001-29999 | 306 | 1,372 | 1,400 | 700 | 2,406 |
| 30000-39999 | 351 | 2,672 | 1,400 | 700 | 2,451 |
| 40000-49999 | 419 | 2,770 | 1,400 | 700 | 2,519 |
| 50000-99999 | 573 | 3,050 | 1,400 | 700 | 2,673 |
| 100000-100000 | 707 | 3,435 | 1,400 | 700 | 2,807 |
| 100001-199999 | 707 | 3,771 | 2,620 | 980 | 4,307 |
| 200000-200000 | 821 | 5,271 | 2,620 | 980 | 4,421 |
| 200001-299999 | 821 | 5,558 | 3,325 | 1,275 | 5,421 |
| 300000-300000 | 838 | 6,558 | 3,325 | 1,275 | 5,438 |
| 300001-399999 | 838 | 6,950 | 3,950 | 1,650 | 6,438 |
| 400000-499999 | 982 | 7,950 | 3,950 | 1,650 | 6,582 |
| 500000-599999 | 1,245 | 8,370 | 3,950 | 1,650 | 6,845 |
| 600000-699999 | 1,532 | 9,140 | 3,950 | 1,650 | 7,132 |
| 700000-750000 | 1,700 | 9,980 | 3,950 | 1,650 | 7,300 |
| 750001-799999 | 1,700 | 10,470 | 4,850 | 2,250 | 8,800 |
| 800000-899999 | 1,500 | 11,970 | 4,850 | 2,250 | 8,600 |
| 900000-1000000 | 1,776 | 12,264 | 4,850 | 2,250 | 8,876 |
| 1000001-3000000 | 1,875 | 13,230 | 4,850 | 2,250 | 8,975 |
| 3000001-5000000 | 2,000 | 13,580 | 4,850 | 2,250 | 9,100 |
| **Deposit (TZS) (agents) Range** | **To Govt** | **Old Customer Fee** | **To AMBT** | **To Agent** | **New Customer Fee** |
| 0 - 20,000,000 | - | - | - | 100 | - |
| **MOBILE BANKING** | | | | | |
| **Withdrawal - Bank to Wallet (TZS)** | **To Govt** | **Old Customer Fee** | | | **New Customer Fee** |
| 1000-100000 | | 500 | | | 1,200 |
| 100000.1-300000 | | 1,000 | | | 2,200 |
| 300000.1-500000 | | 2,000 | | | 3,200 |
| 500000.1-1000000 | | 3,000 | | | 4,200 |
| 1000000.1-3000000 | | 4,000 | | | 5,000 |
| 3000000.1-5000000 | | 4,500 | | | 7,500 |
| **Deposit (TZS) (Wallet to Bank)** | **To Govt** | **Old Customer Fee** | | | **New Customer Fee** |
| 0 - 9,999,999,999 | - | FREE | | | - |
| **Air-time top-up** | - | FREE | | | - |
| **Utility payments** | - | FREE | | | - |
| **Balance inquiry** | - | 300 | | | 400 |
| **Mini-statement** | - | 300 | | | 500 |
| **Full account statement request** | - | 500 | | | 700 |
| **Cheque book request** | - | 600 | | | 700 |
| **AMBT internal transfers (same account holder)** | **To Govt** | **Old Customer Fee** | | | **New Customer Fee** |
| 1 - 5,000,000 | - | - | FREE | | - |
| **AMBT internal outgoing transfers (other account holder)** | **To Govt** | **Old Customer Fee** | | | **New Customer Fee** |
| 1000-750000 | | 500 | | | 750 |
| 750000.1-2000000 | | 500 | | | 1,000 |
| 2000000.1-5000000 | | 500 | | | 1,000 |
| **AMBT External outgoing transfers (Bank to Bank)** | **To Govt** | **Old Customer Fee** | | | **New Customer Fee** |
| 1000-100000 | | 5,000 | | | 3,000 |
| 100000.1-300000 | | 5,000 | | | 3,000 |
| 300000.1-500000 | | 5,000 | | | 3,000 |
| 500000.1-1000000 | | 5,000 | | | 3,000 |
| 1000000.1-3000000 | | 5,000 | | | 3,000 |
| 3000000.1-5000000 | | 5,000 | | | 3,000 |
| **FOREIGN EXCHANGE TRANSACTION** | | | **TZS** | **USD** | |
| Telegraphic Transfer - Normal Customer (SWIFT) | | | N/A | Up to USD 55 | |
| TISS- Normal Customer | | | 10,000.00 | 4.20 | |
| TISS-Staff | | | 6,000.00 | 2.10 | |
| **LOAN PRODUCT LENDING RATES** | | | **TZS** | **USD** | |
| MICRO LOANS (Rahisi Loans) TZS 500,000 to 10,000,000 | | | from 3.0% per month to 6.0% per month Based on risk profile/risk group of client - on reducing balance | N/A | |
| MICRO LOANS TZS 10,000,001 to 35,000,000 | | | from 3.0% per month to 5.0% per month- Based on risk profile/risk group of client - on reducing balance method. | N/A | |
| AGRO LOANS TZS 500,001 TO 35,000,000 | | | from 2.5% per month to 6.2% per month - Based on risk Profile/Risk Group of client - on reducing balance method | N/A | |
| SME LOANS/ODs 35,000,000 to 200,000,000 | | | from 2.2% per month to 2.8% per month- Based on risk profile/Risk Group of client.- on reducing balance method | N/A | |
| Loans/OD Secured by Fixed Term Deposits | | | 20.40% | N/A | |
| **Loan Processing Fee** | | | **TZS** | **USD** | |
| MICRO LOANS (Rahisi Loans) TZS 500,000 to 10,000,000 | | | 3.40%Inclusive of excise duty and VAT | N/A | |
| MICRO LOANS TZS 10,000,001 to 50,000,000 | | | 3.40%Inclusive of excise duty and VAT | N/A | |
| AGRO LOANS TZS 500,001 TO 50,000,000 | | | 3.70%Inclusive of excise duty and VAT | N/A | |
| SME LOANS/ODs 35,000,000 to 200,000,000 | | | 2.90%Inclusive of excise duty and VAT | N/A | |
| Loans/OD Secured by Fixed Term Deposits | | | 1.5% Inclusive of excise duty and VAT | N/A | |
| **Application Fee** | | | **TZS** | **USD** | |
| MICRO LOANS (Rahisi Loans) TZS 500,000 to 10,000,000 | | | 20,000.00 | N/A | |
| MICRO LOANS TZS 10,000,001 to 50,000,000 | | | 20,000.00 | N/A | |
| AGRO LOANS TZS 500,001 TO 50,000,000 | | | 20,000.00 | N/A | |
| SME LOANS/ODs 35,000,000 to 200,000,000 | | | 20,000.00 | N/A | |
| Loans/OD Secured by Fixed Term Deposits | | | 20,000.00 | N/A | |
| **Insurance Fee Annual** | | | **TZS** | **USD** | |
| MICRO LOANS (Rahisi Loans) TZS 500,000 to 10,000,000 | | | 1.5% | N/A | |
| MICRO LOANS TZS 10,000,001 to 50,000,000 | | | 1.5% | N/A | |
| AGRO LOANS TZS 500,001 TO 50,000,000 | | | 2.9% | N/A | |
| SME LOANS/ODs 35,000,000 to 150,000,000 | | | 1.5% | N/A | |
| !"#$%&'()*+,-.+/)01)234+/)5+.6)(+7"%38% | | | 9:;< | )=&>) | |



# Ukosefu wa chumba maalum wasababisha wanafunzi kubadilisha taulo za kike chooni

**Na Shaban Njia,**
SHINYANGA.

WANAFUNZI wa kike katika Sekondari ya Kaselya iliyopo Kata ya Mwamala Halmashauri ya Shinyanga wanatumia moja ya choo shuleni hapo kama chumba maalumu cha kubadilishia taulo za kike.

Wamesema hali hiyo inawapa hofu ya kupata magonjwa mengine yatokanayo na uchafu na kuiomba serikali na wadau kuwajengea chumba hicho.

Walieleza hayo juzi wakati wakizungumza na Nipashe wakati wa utekelezaji wa mradi wa wanajamii na vyombo vya habari katika kutokomeza ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto, unaotekelezwa na klabu ya waandishi wa habari Mkoa wa Shinyanga (SPC) kwa msaada wa Mfuko wa Wanawake Tanzania (WFT).

Mwanafunzi wa kidato cha tatu, Thelezia Jumanne alisema, awali kabla ya kupewa elimu ya matumizi sahihi ya taulo za kike na mwalimu wao wa malezi walikuwa wakitumia vitu ambavyo sio sahihi hususani vitambaa, vidaso, magodoro na vipande vya karatasi hali iliyokuwa ikiwapa miwasho mwilini.

Alisema kwa sasa wameelimika na kuwaelimishwa wazazi wao umuhimu wa taulo za kike, lakini wamekosa mazingira mazuri ya kubadilishia taulo hizo na badala yake wanalazimika kutumia moja kati ya choo cha shule kama chumba maalumu, hali ambayo inawatia hofu ya kupata magonjwa mengine.

Mwanafunzi mwingine, Janeth Mussa alisema wapo baadhi yao wanalazimika kukaa nyumbani na kukosa masomo wakati wa hedhi, kunakosababishwa na baadhi ya wanafunzi wa kiume kuwacheka.

Hivyo, aliomba elimu ya hedhi itolewe kwa wanafunzi wote ili wafahamu.

Mwalimu wa malezi katika shule hiyo, Theodora Mdagachule alikiri uongozi wa shule kutenga moja ya chumba cha vyoo vya wanafunzi wa kike kuwa chumba maalumu kwa kubadilishia taulo za kike.

Alisema hali hiyo imewasaidia kuongeza mahudhulio ya wanafunzi kulinganisha na ilivyokuwa hapo awali.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Kata ya Mwamala, Sophia Philibert alisema, Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Jukwaa la Hedhi Salama imekuwa ikichukua hatua za kukabiliana na changamoto hizo ikiwa ni kuanzishwa kwa kampeni ya kuchangia pedi kwa wanafunzi yenye kauli ya "pedi yangu afya yangu "hivyo wadau wajitokeza kusaidia wanafunzi hasa wenye mazingira magumu.

Alisema elimu inahitajika zaidi kwa jamii ili wazazi na walezi waone suala hilo ni baraka na siyo laana au mikosi, kwani suala la hedhi limezungukwa na usiri mkubwa kiasi kwamba jamii inakosa fursa ya kujadili kwa uwazi namna ya kuliboresha kuanzia ngazi ya kaya hadi jamii nzima.



Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani Wilaya ya Magu, mkoani Mwanza, Mkaguzi Msaidizi wa Polisi, Hossian Jackson (kulia), akitoa elimu ya usalama barabarani na ukatili wa kijinsia kwa wanafunzi wa Shule ya Msingi Igudija, wilayani humo mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Ugonjwa homa ya mapafu wasababisha minada kufungwa

**Na Alex Sayi,** SIMIYU

KUONGEZEKA kwa ugonjwa wa homa ya mapafu na mapele ya ngozi kwa mifugo katika Halmashauri ya Maswa mkoani Simiyu kumesababisha minada kufungwa.

Daktari wa mifugo, Charles Malisa alibainisha hayo juzi mkoani hapa wakati akitoa taarifa ya chanjo ya mifugo katika uchanjaji iliyofanyika katika Kijiji cha Mwanhegele Kata ya Nyabubinza wilayani hapa.

Alisema kutokana na kuibuka na kusambaza kwa ugonjwa huo, wanaendelea kutoa chanjo ili kuikinga mifugo vifo ambayo vimesababisha kufungwa kwa baadhi minada hali iliyoshusha pato la wafugaji.

Alisema hadi sasa mifugo 300,000 tayari imeshachanjwa, huku akitoa wito kwa wafugaji kuendelea kujitokeza ili waweze kushiriki katika uchanjaji wa mifugo yao.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Paulo Maige alisema wafugaji wanapaswa kuona umuhimu wa kuchanja mifugo yao kwani itawasaidia kuwa na ufugaji wenye tija utakaowasaidia kujikwamua kiuchumi.

Aidha, aliwataka wafugaji kupitia chama chao cha CCWT kushirikiana na Serikali ya Wilaya kutatua matatizo yanayowakabili ili kuimarisha ushirikiano baina yao na serikali.

Katibu wa CCWT, Samwel Kidima alisema wafugaji hawana malisho, maji na masoko huku akitoa wito kwa wafugaji ambao bado hawajajiunga na chama hicho kujiunga ili waweze kunufaika na mikopo kutoka taasisi za fedha.

Mmoja wa wafugaji hao, Malale Mbizo akizungumza kwa niaba ya wenzake alisema serikali inapaswa kuendelea kutoa chanjo hizo ili kuwasaidia wafugaji kuikinga mifugo yao na magonjwa, hali itakayowasaidia wafugaji hao kuwa na ufugaji wenye tija.

# Wasichana 23 kati ya 100 wanaugua saratani shingo ya kizazi

**Na Waandishi Wetu**

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu amesema ugonjwa wa saratani ya shingo ya kizazi unazidi kukua kwa kasi nchini na kuwatesa wananchi, kati ya wagonjwa 100, 23 wanabainika kuwa na ugonjwa huo.

Aliyasema hayo juzi wakati akizindua kampeni ya utoaji chanjo hiyo kwa wasichana wenye umri kuanzia miaka 9 hadi 14 jijini Mwanza.

Alisema takwimu zinaonyesha ugonjwa huo unaongoza na kufuatiwa na saratani ya mfumo wa chakula ambayo ni asilimia 11, saratani ya matiti asilimia 10.4 na saratani ya tezi dume asilimia 8.9.

Alisema serikali imeamua kuzindua dozi moja, kwamba awali walikuwa wakipewa wasichana kuanzia umri wa miaka 14, lakini baada ya kutafakari kwa kina ongezeko hilo na kubaini baadhi ya watoto wanaanza kijihusisha na ngono katika umri mdogo, hivyo wakaamua chanjo hiyo kutolewa kwa wasichana wa miaka 9 hadi 14 wakiamini rika hilo litakuwa bado hawajaanza kijihusisha na ngono.

"Ndugu zangu naomba niwaambie saratani ni gharama sana kuliko chanjo, tukubaliane Watanzania leo tunaenda kuikomesha saratani kwa mabinti zetu, tuugue sisi ambao hatujapata fursa ya kupata chanjo, serikali itaendelea kutoa elimu, hamasa kwa wazazi na watoto wenyewe" alisema.

Mwakilishi wa Shirika la Umoja wa Mataifa linalohudumia Watoto (UNICEF) nchini, Elke Wisch alisema kutokana na saratani ya shingo ya kizazi kuendelea kuwa chanzo kikubwa cha vifo lakini wanatambua jitihada za serikali katika kuboresha upatikanaji wa chanjo ya ugonjwa huo nchini ili kuwakinga wasichana dhidi ya magonjwa hayo.

Alisema hadi sasa, chanjo ya HPV kwa dozi ya kwanza imefikia asilimia 79, kipimo cha pili ni asilimia 60, akisema juhudi za pamoja zinahitajika ili kuhakikisha kila msichana nchini anapata ulinzi muhimu dhidi ya saratani ya mlango wa kizazi.

Alisema kampeni hiyo inatoa fursa ya kuwafikia wasichana wengi zaidi na chanjo ya HPV na kuhakikisha hakuna msichana anayeachwa nyuma.

Ofisa Mawasiliano kutoka UNICEF, Usia Ledama alisema chanjo hiyo inalenga kuwafikia wasichana milioni tano wenye umri wa kati ya miaka 9 na 14, kwamba baada ya kuzinduliwa itaendelea kutolewa kwa siku tano.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Anamringi Macha, akizungumza wakati wa uzinduzi wa cjanjo hiyo mkoani Shinyanga alitoa tahadhari kwa wananchi wanaopotosha utoaji wa chanjo hiyo, akisema yeyote atakayebainika atachukuliwa hatua kazi za kisheria.

Alisema mkoani Shinyanga chanjo hiyo itawafikia wasichana 198,865 itatolewa hadi Aprili 28 mwaka huu.

Alisema: "Chanjo hii ni salama kabisa na haina madhara yoyote, na ilianza kutolewa tangu mwaka 2014, tangu kipindi hicho hakuna madhara yoyote ambayo yametokea, sasa kwa wale ambao wataanza upotoshaji serikali itawachukulia hatua," alisema Macha. Aidha, alisema serikali haiwezi kuleta chanjo yenye madhara kwa wananchi wake ambapo chanjo hiyo imethibitishwa na Shirika la Afya Duniani (WHO), pamoja Wizara ya Afya kupitia Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba Tanzania (TMDA), kuwataka wazazi wasiwe na wasiwasi dhidi ya chanjo hiyo.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Dk. Yudas Ndungulile, alisema tayari chanjo zote zipo kwenye vituo, kwamba zitatolewa katika maeneo ya shule za msingi na sekondari, pamoja na kwenye vituo vya afya.

Alisema wanatarajia kuwafikia wasichana 198,865 wenye umri wa kuanzia miaka 9-14 na watapewa dozi moja tu.

**Imeandaliwa na Neema Emmanuel (Mwanza) Marco Maduhu (Shinyanga)**


Ukurasa 12

**Ndivyo Mwenyekiti BAVICHA Taifa, anavyochambua sakata ukosefu ajira**


Ukurasa 13

Mwami Tereza Ntare; Kielelezo cha hitaji la kuandika upya historia ya wanawake Tanzania

siasa
JUMATANO APRILI 24, 2024
Nipashe
HABARI BORA NA KAMILIFU


Ukurasa 14

**Kufariki Jenerali Ogolla; kitanzi helkopta yaendelea kuua vigogo**

# Kinana anawageuzia kibao, awasuta wanaokoromea viongozi hadharani

**Na Maulid Mmbaga**

• Aonya wasiparamiwe kwenye mikutano



Makamu Mwenyekiti wa CCM Bara, Abdulrahman Kinana, akizungumza na wana CCM wa Mkoa wa Mara. **PICHA: MAULID MMBAGA**

MAKAMU Mwenyekiti wa CCM Bara, Abdulrahman Kinana, anawakumbusha wana-CCM, kuwa kuelekea uchaguzi wa Serikali za Mitaa na uchaguzi mkuu wa 2025,umoja na mshikamano katika utendaji kazi ni muhimu na kwamba tofauti miongoni mwao zitawarudisha nyuma badala ya kuwapeleka mbele.

Anawaambia:"Ukiona mtu anafanya vitu ambavyo si sawa hayo ni yake, pia tunaelekea kwenye uchaguzi ili tushinde viongozi lazima mtende haki tusimpendelee mtu, tusipandikize watu wala kupokea rushwa kwani ni adui wa maendeleo na malengo yetu."

Anatoa angalizo hilo ,mkoani Mara kwenye ziara iliyolenga kukagua utekelezaji wa ilani ya CCM, akieleza kwamba endapo mifumo ya ndani ya chama itafanya kazi kikamilifu wataendelea kuwa na nguvu, kuaminika na kukubalika na umma. Anasema chama hicho kinaendeshwa kwa kufuata katiba, na kwamba kina kanuni kwa kila jambo ikiwamo uchaguzi, maadili na utumishi, akisisitiza kuwa ndani ya CCM kila kitu kinaangaliwa na kinaandikwa kwa utaratibu maalum.

### AWATETEA VIONGOZI

Anawakemea baadhi ya viongozi wa CCM kuwadhalilisha watendaji wa halmashauri hadharani akieleza kuwa kama wana jambo wawaeleze madiwani, wenyekiti wa halmashauri, wakuu wa wilaya na wabunge, kwakuwa viongozi hao wanafanya kazi kwa kuzingatia kanuni za utumishi.

Anawasifu wakurugenzi kuwa wanafanya kazi nzuri na wanapolaumiwa wanabaki kusononeka kwa sababu hawana pakusemea, akisisitiza kwamba wanastahili kupewa heshima zao kama binadamu na watumishi kulingana na kazi wanazofanya.

Kinana anashauri inapobainika wakurugenzi hao wamekosea hawapaswi kuparamiwa kwenye mikutano ya hadhara bali mifumo ya kiutumishi inapaswa kuzingatiwa katika kuwawajibisha na si utaratibu unaotumika wa kuwasema hadharani.

"Usisimame kwenye mkutano wa hadhara ukaanza kumdhalilisha mtendaji wa serikali ambaye ni sehemu ya serikali ya CCM kwa jambo ambalo hata huna ushahidi au ni uzushi. Serikalini kuna utaratibu. Njia ya mawasiliano kati ya chama na halmashauri ni kupitia wenyeviti na wakuu wa wilaya.

"Wanastahili heshima ...Siajabu wakati mwingine mambo unayoyaagiza kwenye kanuni hayakoe watakusikiliza, watarudi nyumbani na kuendelea kufanya shughuli zao nyingine," anasema Kinana.

"Mnapokwenda kukagua miradi msianze tena kutoa kauli za kukashifu watu, ukiona kuna mapungufu mahali, muulize mkuu wa wilaya au mwenyekiti wa halmashauri, nao watamtafuta mkurugenzi watazungumza naye, lakini ukiitaja halmashauri wakati kuna serikali watakosa nguvu ya kufanya kazi, nawasihi tuache tabia hiyo wote tunakosea," anasisitiza Kinana.

Kinana anasema hafurahishwi na namna watendaji hao wanavyoshambuliwa, akishauri kama mambo hayaendi sawa waende kwenye ofisi zao kuomba ufafanuzi badala ya kuwasema bila kujua jambo kwa kina.

### VIKUNDI KUCHAFUANA

Katika hatua nyingine Kinana anabainisha kuwa kuna baadhi ya wana CCM wanaotengeneza vikundi vya Whatssap vinavyotumika kudhalilishana, kutuhumiana na kusemana vibaya.

Alidhani vikundi hivyo ni vya kutengeneza na kuelezana habari njema za chama na shughuli za maendeleo, lakini anashwangazwa vinatumika kushambulia watu, akishauri visitumike kudhalilishana, kutuhumiana na kusemana vibaya.

"Nadhani itabidi tutengeneze utaratibu ndani ya chama chetu, hatuwezi kuwa na chama ambacho kuna vikundi, halafu mtu akikukosea humo humo kwenye kikundi unaanza kumsema vibaya na wewe au yeye inabidi ajibu." Anaongeza.

"Tena mnawagawa watu. Anaulizwa uko wapi wewe upo na mimi au na yeye? Akisema siko na yeyote anaambiwa hapana basi kama hauko na yeyote uko na mimi," anaeleza.

Makamu Mwenyekiti Bara anasisitiza wanachama kushikamana kwa umoja, akieleza kuwa atawaomba wakuu wa wilaya wamtafutie madalali ambao hawataki utulivu wanaochochea mote ili watu wafarakane.

"Kuna watu mahali kukitulia wanakosa raha, mpaka wachochee, wakimuona diwani anafanya kazi vizuri hawakubali mpaka wamtafutie wa kumpinga, waambieni waache hizo kazi," anaeleza Kinana

Anawataka wenyeviti wa wilaya na mikoa endadapo wataona mtu anajiandaa na uchaguzi kwa kuanza kampeni kabla ya muda wamdhibiti kwasababu kanuni za maadili zipo.

"Mkiona mtu anatafuta nafasi ya mtu ambaye tayari nafasi hiyo ina mtu msimcheleweshe, tunataka nchi itulie mkiweka nguvu zenu katika kupambana kuleta maendeleo tutapiga hatua," anashauri Kinana.

Katika mkutano huo, mjumbe wa Kamati Kuu ya Taifa CCM, (NEC), Mkoa wa Simiyu, Emmanuel Silanga, anasema ili chama hicho kitekeleze ilani yake kwa kuzingatia mahitaji ya wananchi mshikamano baina ya chama na watendaji wa serikali ni muhimu.

"Mnajua tunakwenda kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa na mkuu ilitufanikishe jambo hili ni lazima madiwani na wabunge watekeleze ahadi kwa kuzingatia ilani ili tuendelee kupata urahisi ...chama kushika dola," anasema Silanaga.

Mwenyekiti wa CCM, Mara, Patrick Chandi, anasema mkoa huo umepokea Shilingi bilioni 600 kutoka serikalini kutekeleza miradi ya maendeleo na kwamba wanachohitaji ni ushirikiano wa viongozi wa CCM na serikali kuisimamia.

"Tunachohitaji hapa ni usimamizi kwa viongozi wetu kuanzia madiwani kwa sababu ilani ni mkataba na wananchi, tukisimamia vizuri tutaendelea kushinda na tutazidi kukiongezea chama chetu nguvu na mapato," anasema Chandi.

# Ndivyo Mwenyekiti BAVICHA Taifa, anavyochambua sakata ukosefu ajira

## • Ajiandaa kurudi Nyamagana kuusaka ubunge 2025

Na Enock Charles

CHADEMA ni miongoni mwa wadau wa kisiasa wanaoshiriki kuibua mawazo mbadala katika ujenzi wa Taifa kikiwa ni chama kikuu cha upinzani, hususani kukabiliana na shida ya ukosefu wa ajira kwa vijana.

Mwenyekiti wa Baraza la Vijana BAVICHA, John Pambalu, anazungumza na Nipashe katika mahojiano maalumu kueleza kuhusu juhudi za chama hicho chenye ushawishi mkubwa nchini miongoni mwa vile vya upinzani. Endelea...

**SWALI: Unalizungumziaje tatizo la vijana kukosa ajira, ukiwa katika taasisi mojawapo ya kuongoza vijana?**

**JIBU:** Dunia leo iko kibiashara na sisi CHADEMA tunaamini katika biashara. Mrengo wetu ni wa kati au ni kiliberali, huko soko linaamuliwa na mahitaji ya bidhaa na uzalishaji au upatikanaji. Kazi hizo zinahusisha rasilimali watu viwandani na kwenye huduma hivyo kwa sababu tumebadilika tunategemea soko liongoze uchumi.

Soko linaleta mabadiliko na namna ya kupata ajira, zamani tulikuwa na mpira wa kujitolea leo ni wa kulipwa kwa hiyo kila binadamu anastahili ujira kwa kazi anayoifanya na siyo kujitolea.

Kwenye sera yetu ya vijana, tutatumia sekta binafsi kutatua changamoto ya ukosefu wa ajira, kwa mfano tumeandaa namna ambavyo kijana anayeanza biashara hapaswi kutozwa kodi kwanza, yaani leo ndiyo anaanza na hapo hapo analipa kodi, ni lazima upewe muda maalum kujitafuta.

Lakini pia, tumeamua katika kila benki kutakuwa na dirisha maalum la kutoa mikopo kwa vijana. Aidha, benki zote za kibiashara zitatoa elimu ya biashara kwa vijana ili wawe na uwezo wa kurudisha mikopo na riba na kulipa kodi tofauti na sasa ambapo jukumu hilo sasa halijapewa kipaumbele.

**SWALI: Tuambie BAVICHA mnapata wapi fedha za kufanyia harakati zenu?**

**JIBU:** Chama kinatoa mchango wa fedha kwenye baraza, lakini pia tuna wanachama ndiyo wadau namba moja wa kuchangia kazi zetu, tumetengeneza wadau ambao ni vijana wenye umri wa chini ya miaka 35. Kwa ujumla vijana ndani na nje ya nchi ndiyo wahusika wakuu.

Wengine wapo katika taasisi binafsi, kuna diaspora hao wamekuwa na mchango mkubwa sana katika baraza letu. Tumelifanya kuwa la wanachama ili wajione wanamiliki. Matukio kama ya Siku ya Vijana Duniani yanagharimu mamilioni ya fedha na vijana ndiyo wanaoyafanikisha.



John Pambalu, Mwenyekiti wa BAVICHA katika majukwaa ya kisiasa. **PICHA: MTANDAO**

> Ikumbukwe baada ya uchaguzi 2020 zaidi ya wanachama wetu 417 walikuwa wafungwa na mahabusu katika magereza mbalimbali.

**SWALI: Ni yapi mafanikio katika uongozi wako BAVICHA?**

**JIBU:** Yako mengi, kwanza tumeandika sera ya vijana ya mwaka 2020 ambayo ina majibu ya matatizo mengi hasa ya kiuchumi yanayowakabili. Pia katika kipindi changu tumelifanya baraza kufanya harakati za kisiasa, bila kuegemea chama. Hapo zamani lilikuwa linafanya shughuli kwa kujificha kwenye chama, mfano kikienda sehemu fulani ndipo unawaona na BAVICHA.

Sisi tumeondokana na hali hiyo na katika mambo fulani tunaweza kusimama kupigania yale tunayoyaona yanahitaji kuzungumziwa na kupatiwa majibu kwa ajili ya jamii yetu. Kwa mfano, BAVICHA ilianzisha harakati ya kutembelea wafungwa magerezani na kupaza sauti ya kutaka kuachiwa kwa wafungwa wa kisiasa.

Ikumbukwe baada ya uchaguzi 2020 zaidi ya wanachama wetu 417 walikuwa wafungwa na mahabusu katika magereza mbalimbali.

Kwa hiyo kwenye harakati tuliweza kujipambanua wenyewe kwamba tunamudu kupigania haki bila kuegemea chama moja kwa moja. Katika oparesheni katiba mpya pamoja na kibano kikali cha uongozi wa hayati John Magufuli na kutuziba midomo, bado BAVICHA ilizunguka katika vijiji mbalimbali kuhamasisha na kutoa elimu ya katiba mpya. Aidha, tumehamasisha vijana kugombea nafasi mbalimbali za uongozi kwa mfano tumekuwa na wagombea vijana kwenye ngazi ya ubunge, kama Mwenyekiti nikiongoza kwa vitendo niligombea jimbo la Nyamagana, Julius Mwita aliyekuwa Katibu Mkuu wa baraza aligombea Musoma Mjini, Patrick Ole Sosopi alikuwa Isimani, Aisha Madoga Dodoma Mjini, Hadija Mwago Mbagala, na Neema Chozaile Geita Vijijini.

Kadhalika, tumewahamasisha vijana kushika nafasi za juu za maamuzi ndani ya chama, kwa mfano Mkoa wa Simiyu aliyekuwa Mwenyekiti wa Vijana Mkoa ndiye Mwenyekiti wa CHADEMA na katibu wake ndiye Katibu wa chama. Katika mikoa ya Mwanza na Kagera, vijana wametoka kwenye uongozi wa vijana kwenda uongozi wa chama kwa kifupi wameiva na wanaaminika.

Aidha, BAVICHA ninayoiongoza imeweza kuwafikia vijana wasomi wa vyuo vikuu na sasa wameingia kwenye siasa kwa kiwango kikubwa. Kamati tendaji ya baraza ninayoiongoza imeacha woga. Zamani vijana wasomi wa vyuo vikuu katika mikoa yote tulikuwa si zaidi ya watano, leo mambo yamebadilika.

**SWALI: Umefanikiwa vipi kukabiliana na changamoto BAVICHA?**

**JIBU:** Bado kuna shida ya ushiriki mdogo wa vijana wasomi katika siasa kwa kuhofia hatma zao katika ajira na mustakabali kwenye maisha. Wakati sisi tunaingia madarakani vijana wa vyuo vikuu walioanzia uongozi katika CHASO (CHADEMA Students Organisation), tulikuwa wachache hatukuzidi watano.

Hata hivyo, hali imebadilika kwa kiasi kikubwa, mathalani, viongozi wapya waliochaguliwa sasa katika wilaya na mikoa asilimia 80 wanatokea CHASO.

Kwa hiyo, tumefanikiwa kushawishi vijana wa vyuo vikuu kufanya siasa. Ni wazi kwamba wale waliokuwa wanadhani wakiingia kwenye siasa hawataajiriwa huo woga umetoweka, katika wachache waliokuwepo walikuwa wanawaza kwenda kwenye ubunge na udiwani, lakini sasa wameona wanawajibu wa kujenga taasisi yetu CHADEMA.

**SWALI: Ni upi mwelekeo wako kisiasa katika siku zijazo?**

**JIBU:** Ni kuendelea kukitumikia chama na wananchi katika nafasi yoyote watakayonipa, lakini pia nina mpango wa kurejea kugombea ubunge katika jimbo la Nyamagana 2025. Nina uhakika nitashinda na kuongoza wananchi kutatua changamoto mbalimbali zilizopo Nyamagana kwa sasa.

**SWALI: Una maoni gani kuhusu sheria mpya za uchaguzi zilizopitishwa karibuni?**

**JIBU:** Hii tunaweza kuita kupaka rangi kuficha ukweli lakini kimsingi hakuna mabadiliko tuliyotarajia na kimsingi hatuziungi mkono. Wameandaa Sheria ya Tume Huru ya Uchaguzi wakati katiba haiitambui inachokilinda ni Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Tunaona ni kukinzana sheria na katiba. Ikumbukwe popote panapokuwa na ukinzani, katiba ndiyo inayotumika.

Jambo la pili, uhuru wa tume siyo jina ni muundo na sisi tumekuwa tukipinga tume ya uchaguzi kuwa na watumishi wa umma tunataka iwe na maofisa wake kuanzia ngazi ya chini mpaka za kitaifa kwa ajili ya uchaguzi ulio huru na haki. Wametoa jina wakurugenzi na kuandika Ofisa Mwandamizi wa Serikali hapo wanacheza na akili za watu. Wakurugenzi ni maofisa waandamizi wa serikali ukweli unabaki kuwa matatizo ya tume si ya kisheria ni ya katiba. Watu wanataka kuwe na mgombea binafsi, katiba inakataa, wanataka haki ya kupinga matokeo ya urais mahakamani, sheria imekataza kwa hiyo vitu vingi bado haviko sawa. Vilevile watu tuliamini kwamba itakapotungwa sheria ya Tume Huru ya Uchaguzi, itatumika uchaguzi wa mwaka 2025 lakini, inataka wajumbe wa tume waliopo sasa kuendelea kusimamia uchaguzi hadi utumishi wao utakapokoma.

MWANASIASA MWAMI TEREZA NTARE

# Kielelezo cha hitaji la kuandika upya historia ya wanawake wa Tanzania

**Na Mwandishi Wetu**



Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Damas Ndumbaro (aliyekaa kulia), katika Maadhimisho ya Mafanikio ya Mwami Tereza, pamoja na wadau mbalimbali kuenzi michango yake na ya wanawake walioshiriki katika harakati za ukombozi wa Tanganyika. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

MWAKA 1958 uchaguzi unafanyika ili kumpata kiongozi mkuu wa machifu wote wa Tanganyika. Zilikuwa zama za ukoloni wa Waingireza na mwanamama Mwami Tereza Ntare II, Chifu wa Jamii ya Heru wa Kigoma anaibuka kidedea. Akiwaangusha machifu wanaume.

Wakati huo Tereza alikuwa chifu pekee mwanamke na kwa kura nyingi anachaguliwa kuwa Mkuu wa Machifu wote Tanganyika, akichuana na Chifu Marealle wa Marangu mkoani Kilimanjaro.

Kuanzia zama hizo hadi sasa ni miaka 66, licha ya leo kuwapo teknolojia na hata ushiriki wa wanawake katika siasa kuongezeka tofauti na wakati wa ukoloni, cha kushangaza idadi ya kinamama inazidi kuporomoka kwenye uwanja wa siasa na mara nyingi wakigombea uchaguzi majimboni wanashindwa.

Ni tafakuri inayoibuka kwenye jukwaa la kusherehekea mafanikio ya Mwami Tereza Ntare linaloandaliwa na Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake, Makumbusho ya Taifa na familia ya Tereza, jijini Dar es Salaam hivi karibuni.

Mgeni rasmi kwenye maadhimisho hayo akiwa Waziri wa Utamaduni Sanaa na Michezo, Dk. Damas Ndumbaro, anawatafakarisha washiriki wa maadhimisho hayo akihoji:

"Ikiwa mwaka 1958 mwanamama Mwami Tereza alishinda uchaguzi kwa kura nyingi kwa asilimia 89 na kuwa kiongozi wa machifu, nini kilifanyika wakati huo? Leo kikwazo nini idadi ya wanawake kwenye uchaguzi haijaongezeka?

Anasema kuna mengi ya kujifunza, mojawapo ni ujasiri, uthubutu , upambanaji na kujiamini.Anawaambia washiriki kuwa wanawake wanaweza kupata ukombozi kwa kufanya mambo hayo na pia kuungwa mkono na jamii kama Tereza alivyoungwa mkono na jamii ya machifu wa Tanganyika wakati huo.

Anamwita Mwami Tereza shujaa ambaye licha ya kusoma Ulaya alicha masomo na kurudi ili kuongoza jamii na taifa lake, baada ya kifo cha baba yake mwaka 1947, akiwa ni mzalendo aliyejali maslahi ya wengi na siyo yake.

Anasema licha ya kwamba historia yake haifahamiki ni mwanamke wa kwanza kujiunga na chama cha TANU na kuieneza kwa watu wa Ukanda wa Magharibi ya Tanganyika.

Aidha, alishirikiana na machifu wengine kueneza ujumbe wa TANU wa kuleta uhuru wa Tanganyika .

Waziri Ndumbaro anasema kazi za mwami Tereza ni alama ya kishujaa inayoonyesha uvuwa wapo wanawake wana mapinduzi, wapigania uhuru waliojitoa kuleta uhuru wa Tanganyika na Afrika ili kuwaondoa watu kwenye ukoloni.

### KUANDIKA HISTORIA

Akizungumzia kazi za Mwami Tereza kukosekana kwenye historia ya Tanzania, Dk. Ndumbaro anasema:

"Ni kutokana na sisi kutoandika kazi zetu, tuondoe uvivu hata sasa tunawaachia wengine waandike historia yetu kwenye mitandao."

Nitoe mfano" "Kulikuwa na ziara ya kiongozi mashuhuri kutoka Marekani aliyekuja Tanzania na taarifa kwenye mitandao zikaripoti kuwa kiongozi huyo anatembelea kijiji cha wavuvi cha Dar es salaam. ....is visiting the largest fishing village of Dar es salaam"

Anasema huo ni upotoshaji, unaotokea kwa sababu watu hawaandiki wenyewe historia matukio , harakati na masuala yote yanayolihusu taifa.

Ili kuondoa upotoshaji na hata kutoandikwa kwa kazi za kishujaa kama ilivyotokea kwa Mwami Tereza watu waanze kuandika sasa.

Akireja uchache wa wanawake kwenye uwanja wa siasa, Mkurugenzi wa Shirika la Women Fund, Rose Marandu, anasema wanawake waliochaguliwa katika uchaguzi mkuu wa 2020 ni 26 pekee kati ya 264 waliopigiwa kura majimboni.

Akitazama uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika mwaka huu, ukifuatiwa na uchaguzi mkuu mwakani, Rose anatoa angalizo.

Anasema chaguzi hizo zinajiri wakati wanawake kwenye sekta ya uongozi wa serikali za mitaa ni ndogo mno, ni asilimia mbili pekee ya wenye viti wa vijiji na asilimia 6.7 ya wenye viti wa vitongoji.

Kwa mujibu Ofisi ya Takwimu ya Taifa (NBS), Tanzania ina vijijini 12,319, vitongoji viko 64,384 wakati mitaa ni 4,263.

Kwa idadi hiyo ya vijiji, wanawake wenyeviti ni wachache mno ni takribani 246 pekee kwa Tanzania nzima, Rose akitafsiri hali hiyo kuwa kukosa uwiano na kuzidi kukwamisha jitihada za kufikia usawa kwa uwakilishi wa 50/50 baina ya wanawake na wanaume kwenye uongozi na uwakilishi.

Anaishauri serikali kuona umuhimu wa kutoa hamasa na elimu kwa wanawake ili waweze kufikia ndoto zao , kuweka mazingira na miundombinu wezeshi ili kuwafikisha kwenye ushiriki wa masuala ya kisiasa, kijamii na kiuchumi ili kupata viongozi kama Mwami Tereza.

> Ni kutokana na sisi kutoandika kazi zetu, tuondoe uvivu hata sasa tunawaachia wengine waandike historia yetu kwenye mitandao.

### MAMBO MAKUBWA

Katika maadhimisho ya mafanikio ya Mwami Tereza, mambo mengi aliyoyafanya yalibainishwa kwa mfano, alinunua kadi 3,000 za TANU na kuzisambaza kwa wananchi usiku wa manane, huko Kigoma ili washiriki uchaguzi mkuu wa 1958.

Taarifa zake zilimfikia Mkuu wa Wilaya ya Kasulu DC mkoloni wa Kiingereza aliyevamia nyumba yake na kutaka kuipekua.

Mwami alidaiwa kukuwsanya kadi na kuzilalia akihoji inakuwaje apekuliwe usiku, hata hivyo DC na jeshi lake walikimbia baada ya wananchi kujipanga na silaha za jadi kukimbilia nyumbani kwa Tereza kumnusuru baada ya kusikia kuwa amevamiwa usiku wa manane.

Kutoa kadi hizo kuliwezesha watu kuzitumia kupiga kura mwaka 1958 na kukipa chama cha TANU ushindi mkubwa.

Mwami Tereza anatajwa kuwa msomi wa sheria aliyejua haki za binadamu na kuzitetea alitumia elimu yake kueneza TANU mikoa ya Tabora, Shinyanga na Rukwa pia alishiriki katika misafara ya kuomba kura, kuhimiza watu kuiunga mkono TANU na kuwashawishi machifu wengine kushiriki kwenye harakati za kupigania uhuru.

Aidha, anatajwa kuwa mwanamke shujaa na alama ya ukombozi wa Tanganyika, ambaye baada ya chama cha TANU kuanzishwa 1954, alikuwa mwanamke wa kwanza kujiunga akiwa mstari wa mbele kueneza kwa machifu wengine.

Kiongozi huyo ambaye licha ya machifu kukatazwa kujihusisha na siasa kwa sheria iliyotungwa na wakoloni alisimamia ustawi wa TANU na kuiimarisha.

JUKWAA LA VIONGOZI

# Kufariki Jenerali Ogolla; kitanzi helkopta yaendelea kuua vigogo

• Yumo Saitoti, ndege kadhaa za Uganda zikiangushwa



Enelo ilipoanguka helkopta iliyombeba aliyekuwa Mkuu wa Majeshi ya Kenya pamoja na maofisa wengine. **PICHA: MTANDAO**

**Na Sabato Kasika**

KWA familia, Jeshi la Ulinzi la Kenya (KDF) na taifa zima ni kilio kutokana na wiki kumalizika na kifo cha Mkuu wa Majeshi, Jenerali Francis Ogolla na baadhi ya maofisa wa ngazi za juu wa jeshi waliopoteza maisha kwenye ajali ya ndege.

Ogolla na wenzake walikuwa kazini katika ziara ya kukagua vikosi vya askari wanaopambana na mauaji ya raia, wizi na kutorosha mifugo .

Tukio hilo lilitokea Alhamisi Aprili 18, na kumuua mkuu wa KDF, katika eneo la Marakwet, umbali wa kilomita takriban 400 kutoka Nairobi.

Kuanguka kwa helkopta aliyopanda Jenerali Ogolla na kupoteza maisha yake na ya maofisa wenzake nane, wakati wakitembelea vikosi vya kijeshi vinavyopambana na uhalifu, ikiwamo wa wizi wa mifugo kunaandika historia nyingine ya vifo angani nchini humo.

Itakumbukwa Mkuu wa Majeshi anafariki dunia kwenye helkopta ikiwa ni miaka 12 tangu kiongozi mwingine Waziri wa Mambo ya Ndani wa nchi hiyo Profesa George Saitoti kufariki dunia kwa ajali ya usafiri kama huo.

Pamoja na maofisa wengine Profesa Saitoti alifariki na Naibu wake Peter Orwa Ojode, wakiwa kwenye safari ya kushiriki tukio la kijamii kijijini kwa Naibu huyo.

Ndege yao ilianguka na kuwaka moto na taarifa kuwa ilikuwa na sumu ambayo ilisababisha kukosa hewa safi na kupoteza maisha ya viongozi hao zikiwa zimezagaa japo hazikuthibitishwa .

> “Inaelezwa kuwa helikopta hiyo ilikuwa imetua katika uwanja wa shule moja, baada ya muda au dakika chache ikapaa, lakini ikashindwa kuendelea na safari na kuanguka kisha kuua watu saba na kujeruhi wawili.



Aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani, Prof. George Saitoti



Aliyekuwa Mkuu wa Majeshi ya Kenya, Francis Ogolla

Kinara na mbobezi wa mahesabu Profesa Saitoti alikuwa msomi, mtaalamu wa fikra tunduizi mchumi na mbobezi wa masuala mengi ya kisayansi, alikufa wakati taifa hilo likiongozwa na Mwai Kibaki.

Mkasa huo ulitokea June 10, 2012, na kusababisha mshangao, huzuni na hofu kwa Wakenya kutokana na kumpoteza kiongozi huyo aliyekuwa pia Makamu wa Rais wa nchi hiyo na watu wote saba waliokuwamo walikufa.

Waliopoteza maisha nao ni walinzi wao na rubani wa helkopta hiyo, iliyokuwa ikielekea Nthiwa nyumbani kwa Naibu Waziri Ojode iliyoanguka katika milima ya Ngon'g nje kidogo ya Nairobi.

Kuanguka na kuungua helkopta hiyo kulitokea baada ya mkasa kama huo kuibuka Juni 10 mwaka 2008 kuwaua, Waziri wa Barabara, Kipkalya Kones na Naibu Waziri katika Ofisi ya Makamu wa Rais Lona Laboso.

Miaka minne baadaye, yaani mwaka 2012 nchi hiyo ilikumbwa tena na tukio lingine la ajali ya helkopta ambayo iliondoa uhai wa aliyekuwa Waziri wa Usalama wa Ndani, Profesa George Saitoti na kuongeza maswali kuhusu helkopta na vifo vya viongozi.

Lakini miezi miwili baadaye, ilielezwa maofisa wa Jeshi la Kenya wakitangaza kupotea kwa helkopta tatu za Uganda ndani ya ardhi ya Kenya zikiwa njiani kuelekea nchini Somalia.

Alikaririwa msemaji wa jeshi hilo Bogita Ongeri, akisema helikopta hizo zilipotea karibu na eneo la Mlima Kenya, lakini rubani mmoja aliweza kuwasiliana nao, akiomba msaada.

Baadaye Agosti 14 mabaki ya helikopta mbili za kijeshi za Uganda yalipatikana katika msitu wa Mlima Kenya zikiwa zimeteketea, na kwamba helkopta ya tatu ilianguka katika mlima huo.

Hata hivyo, inaelezwa kuwa wanajeshi waliokuwa katika helkopta hiyo waliokolewa. Msemaji wa jeshi la Kenya Ongeri, alikaririwa akisema helkopota hizo za kivita zilikuwa zikienda kuimarisha kikosi cha Umoja wa Afrika kukabiliana na kundi la kigaidi la Al-Shabaab.

Ikiwa ni miaka minne kupita tangu kupotea kwa helkopta hizo za Uganda ndani ya nchi ya Kenya, kuanguka kwa helkopta iliyopanda Jenerali Ogolla na maofisa wenzake nane walikuwa katika ziara ya kutembelea vikosi vya kijeshi vinavyopambana na uhalifu, ikiwamo uhalifu sugu wa wizi wa mifugo, linakuwa tena habari ya kusikitisha.

Inaelezwa kuwa helikopta hiyo ilikuwa imetua katika uwanja wa shule moja, baada ya muda au dakika chache ikapaa, lakini ikashindwa kuendelea na safari na kuanguka kisha kuua watu saba na kujeruhi wawili.

**UCHUNGUZI WA AJALI**

Rais wa nchi hiyo, William Ruto anasema, serikali itafanya uchanguzi wa kifo cha Jenerali Ogolla na utawekwa wazi, ili Wakenya wajue chanzo cha ajali ya helkopta iliomuua na maofisa wenzake.

“Ninataka kuhakikishia nchi kwamba wanajeshi wa Ulinzi wa Kenya na Jeshi la Wanaanga wana uadilifu na weledi unaohitajika ili kuhakikisha kuwa hakutakuwa na mashaka yoyote kuhusu kilichompata Jenerali Ogolla,” Rais Ruto anasema.

Katika ujumbe wake, Rais Ruto anamsifia Jenerali Ogolla kwamba alikuwa kamanda mwenye ari ya kufanya kazi na raia mzalendo wa Kenya mwenye unyenyekevu na uadilifu mkubwa.

Wakati akisema hayo, hasimu wake kisiasa Raila Odinga anatupilia mbali madai kwamba Jenerali Francis Ogolla alijaribu kubatilisha ushindi wa William Ruto katika uchaguzi wa Agosti 2022.

Mwanasiasa huyo mkongwe, ambaye aliwahi kuwa Waziri Mkuu wa Kenya kuanzia 2008 hadi 2013, anasema hayo Ijumaa jijini Nairobi wakati wa kumuaga kijeshi marehemu Ogolla.

Jenerali Ogolla ameacha mjane na watoto wawili, alizikwa nyumbani kwake Jumapili iliyopita, kijijini Ng'iya, katika Kaunti ya Siaya.





# Bodi yaagizwa kuanzisha mfuko kusajili wakulima wa korosho

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Kilimo, Hussein Bashe ameiagiza Bodi ya Korosho Tanzania kuanzisha mfumo wa kusajili wakulima wa zao hilo ili kuongeza uzalishaji kutoka tani 350,000 za mwaka huu.

Bashe alitoa agizo hilo jana kwenye kikao cha tathmini ya uzalishaji, ubanguaji na masoko ya korosho kilichofanyika jijini hapa.

Alisema lazima mfumo huo wa kusajili wakulima uwepo kwa sababu ni muhimu kujua shughuli zao za kilimo katika maeneo mbalimbali nchini.

Alisema bodi hiyo ni lazima inatakiwa pia kuwa na idadi ya mikorosho, umri wa miti na wakulima wapewe namba ili waonekane kwenye orodha.

"Anzisheni mfumo wa kusajili wakulima itawasaidia pia kujua wana changamoto gani katika kilimo wanachofanya, " alisema Bashe.

Alisema lengo la serikali ni kuona zao la korosho linapiga hatua na wakulima kuinuka kiuchumi.

Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Brigedia mstaafu Aloyce Mwanjire, alisema wako imara kuhakikisha mnyororo wa thamani wa zao hilo unasonga mbele.

Brigedia Mwanjire, alisema mnyororo wa kuzalisha korosho ghafi unapaswa kuangalia kwa makini ili kuhakikisha soko la zao hilo linapatikana na wakulima wananufaika na kilimo hicho.

Aliishukuru serikali kwa usimamizi mzuri ikwenye kilimo cha korosho na kuwasaidia wakulima kupiga hatua.

# Wasichana 178,144 kupatiwa chanjo saratani ya kizazi

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

WATOTO wa kike wenye umri kuanzia miaka tisa hadi 14 wapatao 178,144 mkoani hapa wanatarajia kupatiwa chanjo dhidi ya ugonjwa wa Saratani ya Mlango wa Kizazi (HPV).

Akizungumza na wananchi na wanafunzi katika Kata ya Kisaki Halmashauri ya Manispaa ya Singida kabla ya kuzindua chanjo hiyo juzi, Mkuu wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, alisema mpango wa serikali ni kuwalinda wanawake dhidi ya kirusi kinachosababisha ugonjwa huo kisiweze kuwapata na kuleta madhara.

"Serikali imewekeza kwa watu wake maana huwezi kuwa na barabara nzuri, shule bora kama watu wake ni wagonjwa na kama mnavyofahamu ugonjwa wa saratani bado ni changamoto unapompata mwanamke mara nyingi ni kifo kwa hiyo mtu anapopewa chanjo hii maana yake anawekewa askari wa kumlinda," alisema Dendego.

Alizitaka timu zote za kampeni kuhakikisha zinawafikia watoto wote wa kike kwenye shule za serikali, binafsi, migodini na mitaani kwani chanjo hii inatolewa bure na haina madhara.

Alisema serikali kupitia Wizara ya Afya na Wizara Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) imewekeza fedha nyingi, hivyo jukumu la wazazi na walezi wenye watoto wao waliofikisha umri huo kutoa ushirikiano ili wakapatiwe chanjo hiyo.

Katibu Tawala wa Mkoa huo, Dk. Fatuma Mganga, alisema kitendo kinachofanywa na serikali cha kutoa chanjo hiyo kwa watoto wa kike ni uwekezaji kwa wananchi wake hususani wanawake ili wawe na afya njema hivyo washiriki vyema katika uzalishaji mali.

Alisema pamoja na vituo vilivyotengwa kwa ajili ya kutolea chanjo, maeneo mengine ya kwenye machimbo ya madini yafikiwe ili wasichana waliopo huko nao wapewe chanjo.

Mganga Mkuu wa Mkoa huo, Dk.Victorina Ludovick, alisema hilo iliyoanza kutolewa mkoani hapa Aprili 22, mwaka huu, itaendelea hadi Disemba mwaka huu kwa watoto hao wa kike.

Dk. Ludovic, alisema chanjo hiyo inatolewa kwa wawake kutokana na Tanzania kuwa miongoni mwa nchi ambazo zinapoteza wanawake wengi kutokana na saratani ya mlango wa kizazi ambao huambukizwa kwa njia ya kujamiana.

"Chanjo hii imeanza kutolewa kwa dozi moja badala ya mbili kwa sababu tafiti zinaonyesha kuwa dozi moja tu inaweza kukinga maradhi hayo kwa mwanamke na ifikapo Januari 2025 chanjo hii itaanza kutolewa kwa wasichana wenye umri wa miaka tisa tu," alisisitiza.

Aliwahiza wanawake kufanya uchunguzi wa afya zao kupitia vifaa vya kitabibu ili kugundua kama wana virusi vya saratani ya mlango wa kizazi na kupata matibabu haraka.

Mtaalamu wa Wizara ya Afya, Nelson Kamuhanda, alisema chanjo hiyo ilianza kutolewa nchini mwaka 2018, serikali imeamua kurejea baada kubaini mikoa mingi ipo chini katika utoaji wake, isipokuwa Kigoma.

Kamuhanda, alisema mwaka 2018 chanjo hiyo ilikuwa inatolewa kwa watoto wa kike wenye umri wa miaka 14 tu kwa sababu hakukuwa na chanjo (dozi) ya kutosha, lakini



Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa, akizungumza wakati akizindua Baraza la Wafanyakazi wa Bodi ya Mfuko wa Barabara na Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini unaotumiwa na Wizara ya Ujenzi na Taasisi zake, jijini Dodoma jana. **PICHA: NEEMA EMMANUEL**

# Waziri Bashungwa awaonya watendaji

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAZIRI wa Ujenzi, Innocent Bashungwa amezindua mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ya miradi na kuwaonya watendaji wanaoshindwa kutekeleza majukumu yao ya kuwaletea wananchi maendeleo.

Bashungwa alisema hayo juzi jijini hapa wakati akifungua Baraza la Wafanyakazi la Mfuko wa Barabara na uzinduzi mfumo huo wa ufuatiliaji na tathmini ya miradi inayotekelezwa na serikali nchini.

Alisema mfumo huo ni muhimu kwa utendaji kazi, hivyo watendaji wote wanapaswa kutumia ili kuwarahisishia kufuatilia tathmini ya miradi.

"Nimezindua huu mfumo naomba ukatumike ipasavyo ili kuleta weredi kwenye taasisi mbalimbali ikiwemo kusaidia kufuatilia miradi ya maendeleo inayotekelezwa kati mbalimbali nchini," alisema Bashungwa.

Akizindua baraza hilo, Bashungwa, aliagiza likatumike kutafuta vyanzo vya mapato na kuboresha vilivyopo na kutumike kutatua changamoto za watumishi na kuzifikisha sehemu husika kupatiwa ufumbuzi.

Alisisitiza taasisi zilizopo chini ya wizara hiyo ambazo hazina mabaraza ifikapo Juni 30, mwaka huu ziwe zimeanzisha na kuzindua.

Akizungumzia kuhusu baadhi ya watendaji kuacha majukumu yao na kuyawasilisha kwa waziri au katibu, alisema hataki kusikia suala hilo na kumtaka kila mmoja kuwajibika kwenye eneo lake.

Bashungu, alisema amekuwa akikuta kazi ambazo zingepaswa kufanywa na watendaji wake ofisini kwake kitendo ambacho hakifurahii hata kidogo na kuwataka wakafanye kazi zao kama walivyoagizwa.

Aliwataka baadhi ya watendaji kuacha tabia ya kunyanyasa watumishi wanapotoa malalamiko ili yafanyiwe kazi.

Alisema wengi wao wakitoa maoni na malalamiko yao, wamekuwa wakitishiwa na kutishwa kuwa hawawezi kupewa safari kutokana kuona kuwa wachongewa.

# TAHOSA wataja chanzo shule mpya kufanya vibaya

**Na Mwandishi Wetu,** SINGIDA

UMOJA wa Wakuu wa Shule za Sekondari Tanzania (TAHOSA) Kanda ya Kati umesema shule mpya kucheleweshewa fedha za ruzuku na ushirikiano hafifu wa wazazi kuchangia chakula cha wanafunzi shuleni kunasababisha ufaulu usioridhisha katika shule.

Mwenyekiti wa TAHOSA Kanda ya Kati, Jeremia Mungwe aliyasema hayo juzi wakati wa Mkutano Mkuu wa mwaka wa umoja huo unaofanyika katika Manispaa ya Singida na kuwashirikisha wakuu wa shule zaidi 400 kutoka mikoa ya Dodoma na Singida.

Wakuu hao wamekutana kufanya tathimini ya hali ya elimu na kupeana uzoefu wa taaluma katika wilaya ambazo zinafanya vizuri kielimu kwa lengo la kuongeza ufaulu kwa shule zao.

Akifungua mkutano huo, Mkuu wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego,alisema kanda hiyo bado haifanyi vizuri kielimu, hivyo ni wajibu wa TAHOSA kujadili tatizo hilo na kutoa mapendekezo kwa serikali nini kifanyike ili kuondokana na tatizo hilo.

"Kila mmoja anatambua kazi kubwa anayofanya Rais Samia Suluhu Hassan na serikali yake kwa kujenga shule mpya, mabweni na vyoo kwa wingi ina maana serikali inakwenda na muda hivyo ni jukumu lenu na nyie walimu kuongeza ufaulu katika shule," alisema.

Aliwataja wakuu wa shule wasiwe wanakaa na madeni ya walimu badala yake wayawasilishe ngazi husika ili walipwe haki zao kwa wakati na kupata moyo wa kufanya kazi yao vizuri.

Aliwataka walimu wakuu wa shule wa masomo ya sayansi watoke maofisini na kwenda kufundisha madarasani kwa lengo la kukabiliana na upungufu mkubwa wa walimu wa hisabati, baolojia, fizikia na kemia.

Ofisa Elimu Mkoa wa Singida, Dk.Elipidius Baganda, alisema hali ya kitaaluma kwenye mkoa huo kwa mwaka jana mitihani yote ya taifa ukiondoa wa darasa la nne, ufaulu umeongezeka ikilinganishwa na miaka ya nyuma.

Dk. Baganda, alisema mkoa unaendelea kujipanga ili kuongeza kiwango zaidi cha ufaulu.





# Serikali yashauri mawakala mbolea kupewa mafunzo maalum

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI imeshauri mawakala na wauzaji wa mbolea nchini kupatiwa mafunzo maalumu kuhusu matumizi sahihi ya mbolea, ili wasaidie kufikisha elimu hiyo kwa wakulima kwa lengo la kuongeza tija kwenye uzalishaji.

Katibu Tawala Msaidizi Uchumi na Uzalishaji Mkoa wa Mbeya, Said Madito aliyasema hayo jana jijini Mbeya alipokuwa anafungua mafunzo ya matumizi ya mbolea za Kampuni ya Minjingu yaliyofanyika jijini Mbeya.

Mafunzo hayo yaliwashirikisha mawakala wa mbolea kutoka katika mikoa minne ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ambayo ni Mbeya, Rukwa, Katavi na Songwe ambapo alisema mawakala hao ni kundi muhimu kwenye uboreshaji wa kilimo.

Alisema endapo wakipatiwa elimu sahihi itakuwa rahisi kuwafundisha wakulima matumizi sahihi ya mbolea kwenye mazao mbalimbali na kuongeza kiwango cha uzalishaji na hivyo kufikia malengo ya serikali ya kuifanya sekta ya kilimo kuchangia asilimia 10 ya Pato la Taifa ifikapo 2030.

"Wenzetu Mamlaka ya Udhibiti wa Viuatilifu na Afya ya Mimea (TPHPA) wameweka utaratibu kwamba hairuhusiwi kwa mfanyabiashara yeyote kuuza viuatilifu kama hajapata mafunzo, sasa na sisi huku kwenye mbolea tuanze kufikilia kwenda huko," alisema Madito.

Alisema kuna baadhi ya maeneo nchini maofisa kilimo hawapo lakini hawa wauzaji wa mbolea wapo kila sehemu na hivyo wakipata mafunzo itakuwa rahisi kufanya kazi inayotakiwa kufanywa na maofisa kilimo.

Mkurugenzi wa Masoko wa Kampuni ya Minjingu, Dk. Mshindo Msola alisema lengo la kampuni hiyo ni kuhakikisha inatoa mafunzo kwa mawakala kuhakikisha wanawauzia wakulima mbolea zinazokidhi mahitaji.

Alisema kila mbolea inayozalishwa inakuwa na malengo maalumu ikiwemo kujibu matakwa ya afya ya udongo ya shamba la mkulima pamoja na mazao ambayo mkulima anazalisha.

Alisema mbolea za minjingu zinafaa kwenye uzalishaji wa mazao mbalimbali yakiwemo ya muda mfupi na ya kudumu kutokana na kwamba ni mbolea za asili ambazo pia zinasaidia kulinda afya ya udongo.

Dk. Msola alisema kwa sasa serikali imefanya jitihada za kupima afya ya udongo katika maeneo yote nchini na ramani zimetolewa na hivyo ni rahisi wakulima kununua mbolea kulingana na afya ya udongo ya eneo lao.

"Sisi huu ni utaratibu wetu kila mwaka kukutana na mawakala wetu kufanya tathimini, kusikiliza kero zao na kuzitatua pamoja na kuwaelimisha kuhusu matumizi sahihi ya mbolea, hawa sisi tunawaona kama ni maofisa ugani," alisema Dk. Msola.

Hata hivyo aliwatoa hofu wakulima kuwa mbolea hazisababishi ugonjwa kwenye mazao kama ambavyo baadhi ya wakulima wa mpunga wilayani Mbarali walikuwa wanaamini kuwa ugonjwa wa virusi ulioshambulia mazao yao ulikuwa unasababishwa na mbolea.

Alisema ugonjwa huo ni wa siku nyingi na mpaka sasa umebainika kusumbua maeneo mengi nchini na hivyo akawataka wananchi kuendelea kuziamini mbolea hizo.

Baadhi ya mawakala walishukuru kwa kuanzishwa mafunzo hayo wakieleza kuwa yatawasaidia kuaminika kwa wakulima wanaonunua pembejeo kwao.

Mmoja wa mawakala hao, Diones Shonde alisema mara nyingi wakulima wamekuwa wakiwahoji maswali mbalimbali ambayo baadhi wamekuwa wakishindwa kujibu na kwamba mafunzo hayo yatawasaidia kukidhi mahitaji ya wateja wao.

Kampuni ya Minjingu inaendelea kutoa mafunzo hayo kwa mawakala katika Kanda mbalimbali nchini ili kuhakikisha elimu hiyo inasambaa nchi nzima.

## Tatizo wanafunzi Iganzo kukaa chini lapatiwa ufumbuzi

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

TATIZO la wanafunzi wa Shule ya Msingi Juhudi iliyopo Kata ya Iganzo katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya kukaa chini na baadhi kubanana kwenye madawati limepungua baada ya serikali kuanza kupeleka samani hizo.

Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Josephat Mwaigaga alisema shule ina wanafunzi 2,414 na kwamba ilikuwa na upungufu wa madawati 244 hali iliyokuwa inasababisha baadhi ya wanafunzi kukaa chini na wengine kukaa zaidi ya wawili kwenye madawati machache.

Alisema kwa sasa serikali imeshapeleka madawati 100 na sasa wamebakiwa na upungufu wa madawati 144 na wameahidiwa na serikali kwamba yanatengenezwa yakiwa tayari yatapelekwa.


Alisema kitendo cha wanafunzi kukaa chini ama kubanana kwenye madawati kinasababisha hata ufaulu wa wanafunzi kushuka na baadhi kutopenda kwenda shule.

Alisema shule hiyo ina idadi ya kutosha ya vyumba vya madarasa lakini baadhi havina madawati na kwamba wanakusudia hayo yatakayopelekwa yatawekwa kwenye vyumba hivyo.

Mkurugenzi wa Jiji hilo, John Nchimbi alisema halmashauri hiyo imepanga kutengeneza madawati zaidi ya 6,000 na kuyasambaza kwenye shule mbalimbali ambazo zina upungufu na kwamba idadi hiyo ya madawati ndiyo yalikuwa yanahitajika.

Alisema waligawa tenda ya kutengeneza madawati hayo ambapo baadhi yanatengenezwa na Chuo cha Ufundi Stadi (VETA) na baadhi yanatengenezwa na mafundi wa mtaani.

Hivyo, aliwataka walimu na kamati za shule kuhakikisha wanatunza vifaa vyote ambavyo vinasambazwa shuleni ili vidumu na kuwasaidia wanafunzi kwa muda mrefu.




Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Kanda ya Nyasa, Mchungaji Peter Msigwa (katikati) akirejesha fomu ya kuwania kutetea nafasi hiyo kwa Katibu wa Chama hicho Kanda, Gwamaka Mbughi (kushoto) katika ofisi ya Kanda hiyo, jijini Mbeya juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wananchi Mbeya hawataki risiti wanapofanya manunuzi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANANCHI mkoani Mbeya wanadaiwa kutokuwa na utamaduni wa kudai risiti wanaponunua bidhaa ama huduma mbalimbali, hali ambayo inasababisha migogoro baina ya wafanyabiashara na maofisa wa Mamlaka ya Mapato nchini (TRA).

Wafanyabiashara walitoa malalamiko hayo juzi wakati maofisa wa TRA walipofanya ukaguzi wa kushtukiza kwenye maduka na kwenye masoko kwa lengo la kuangalia namna wafanyabiashara wanavyotekeleza sheria za nchini.

Mmoja wa wafanyabiashara hao, Mandela Ndelwa alisema baadhi ya wananchi huwa wananunua bidhaa na kuondoka nazo bila kuchukua risiti, hata kama watakumbushwa na wafanyabiashara jambo ambalo alisema linahitaji elimu.

Alisema baadhi huwa wanapuuzia kwa kusema risiti hazina maana kwao zaidi ya bidhaa ambazo wanakuwa wamezinunua na hivyo wakishakabidhiwa bidhaa wanaondoka na kuacha risiti hata kama imeshatolewa.

"Kwa mfano hapa kuna dada amekuja amenunua chombo lakini nilipompatia risiti ameikataa kidai kuwa ni uchafuzi wa mazingira na hivyo akaondoka, sasa hili jambo linatugombanisha na serikali," alisema Ndelwa.

Naye Erick Mwaitege alisema baadhi ya wafanyabiashara hao wakikamatwa na maofisa wa TRA huwa wanarudi nao kwenye maduka na kuwaonyesha sehemu waliponunua bidhaa jambo ambalo linasababisha migogoro.

Alisema wakati mwingine maofisa wa TRA wakifika na wateja hao wanakuta risiti zilishatolewa na kwenye mfumo zinaonekana lakini wateja walizipuuzia na kuziacha.

Meneja wa TRA Mkoa wa Mbeya, Musibu Shaban alisema kwa mujibu wa sheria za nchi ni kosa kwa mfanyabiashara kuuza bidhaa bila kutoa risiti na kwamba akikamatwa kuna adhabu ambazo zinaweza kuwaumiza.

Alisema adhabu zinazotolewa kwa wafanyabiashara wasiotoa risiti ni faini isiyopungua Sh. milioni 1.5 ama mara tatu ya thamani ya bidhaa anayokuwa ameiuza na hivyo akawatajka wafanyabiashara wote kuzingatia.

Alisema fedha zinazokusanywa na serikali kupitia risiti zinatumika kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo ujenzi wa miundombinu ya barabara, afya, elimu na huduma zingine muhimu za kijamii. Alisema wanatambua kuwa kuna matatizo mbalimbali yanayotokana na mashine za kutolea risiti za kielektroniki na hivyo huwa wanapita mara kwa mara kuwaelimisha wafanyabiashara ili wasikiuke taratibu.

"Tunapita kwa lengo la kuwaelimisha wafanyabiashara ili wajitahidi kutoa risiti, tunawaelimisha pia namna ya kufanya wanapobaini kuwa mashine za kutolea risiti zina shida, kwahiyo nawaomba sana watimize sheria ili wasikumbane na adhabu," alisema Shaban.





# Udhamini wa NMB Mkutano Mkuu ALAT wafikia bil. 1.2/-

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

BENKI ya NMB, imekabidhi hundi yenye thamani ya Sh. milioni 120 kudhamini Mkutano Mkuu wa 38 wa Mwaka wa Jumuiya ya Tawala za Mitaa Tanzania (ALAT Taifa), uliofunguliwa jana na W a - ziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tamisemi, Mohammed Mchengerwa kwa niaba ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, ukiwakutanisha washiriki zaidi ya 600.

Kiasi hicho kinachodhamini mkutano wa mwaka huu unaofanyika chini ya kaulimbiu ya 'Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ni Jambo Letu; Shiriki kwa Maendeleo ya Taifa,' kinafanya udhamini wa NMB kwa ALAT Taifa kufikia Sh. bilioni 1.2 katika kipindi cha miaka minane.

Mkutano Mkuu wa ALAT unaowapa fursa viongozi wa Serikali Kuu kutoa maelekezo na miongozo ya kisera kwa watendaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, wakiwamo mameya wa majiji na manispaa, wenyeviti wa wakurugenzi wa halmshauri 184 (za Tanzania Bara), utafungwa Aprili 25 na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi.

Kwa miaka minane sasa, NMB na ALAT zimekuwa na ushirikiano endelevu katika masuala mbalimbali kwa maendeleo ya halmashauri zote nchini, ikiwamo kudhamini na kufanikisha vikao na mikutano mikuu ya mwaka ya ALAT, ambayo kimsingi ndio chachu ya utendaji bora kwa halmashauri hizo.


Akizungumza wakati wa hafla ya makabidhiano hayo iliyofanyika Zanzibar juzi, Ofisa Mtendaji Mkuu wa NMB, Ruth Zaipuna, alisema wanajivunia kuwa wabia wakubwa wa ALAT na kwamba wanathamini heshima ya kipekee wanayopewa na uongozi wa jumuiya hiyo.

Sambamba na udhamini huo, Zaipuna alibainisha kuwa NMB imeandaa mchapalo kwa wajumbe wa Mkutano Mkuu wa ALAT Taifa, akiwakaribisha kushiriki chakula cha jioni pamoja na kujadiliana machache baina ya wajumbe wa ALAT na wafanyakazi wa NMB.

Makamu Mwenyekiti wa ALAT Taifa, Sima Constantine Sima, alishukuru NMB kwa ubia endelevu unaowawezesha kufanikisha vikao na mikutano mikuu ya kila mwaka kwa kipindi cha miaka minane sasa ya udhamini wao.

"Nitumie nafasi hii kuishukuru NMB kwa kutafsiri kwa vitendo juu ya uhusiano mwema, ambapo leo pia imedhamini uzinduzi wa kimapinduzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa Zanzibar (ZALGA), ambayo ni mamlaka sawa na ALAT kwa huku visiwani Zanzibar," alisema Sima.

Pia alishukuru NMB kwa kuandaa hafla ya chakula cha usiku baina ya wajumbe wa Mkutano Mkuu wa ALAT Taifa na wafanyakazi wa NMB, akiamini mchapalo huo utakuwa fursa nzuri si tu ya kubadilishana mawazo, bali pia kufurahi pamoja baada ya kazi.




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna (wa pili kushoto), akikabidhi mfano wa hundi yenye thamani ya Sh. milioni 120, kwa Makamu Mwenyekiti wa Jumuiya ya Tawala za Mitaa Tanzania (ALAT) Taifa, Sima Constantine Sima jijini Zanzibar juzi, kwa ajili ya udhamini wa Mkutano Mkuu wa ALAT ulioanza jana. Wengine ni Ofisa Mkuu Wateja Wakubwa na Serikali wa NMB, Alfred Shao (kushoto), Meneja wa Biashara wa Benki ya NMB Zanzibar, Naima Said Shaame (kulia) na Kaimu Katibu Mkuu wa ALAT Taifa, Mohammed Maje. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Dk. Mwinyi ataja faida ujenzi miundombinu ya shule

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi amesema ujenzi wa miundombinu ya shule ina lengo la kuimarisha sekta ya elimu na kupunguza idadi kubwa ya wanafunzi katika madarasa.

Aliyasema hayo wakati wa ufunguzi wa jengo la Shule ya Hassan Khamis Khafith visiwani hapa ikiwa ni miongoni mwa shamrashamra za Maadhimisho ya Sherehe za Miaka 60 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

Alisema ujenzi wa mindombinu ya elimu nchini unalengo la kuboresha sekta ya elimu iliyoko kwenye mageuzi makubwa ya maendeleo.

Alisema ujenzi huo utasaidia kuboresha kiwango cha elimu na kupunguza msongamano mkubwa wa wanafunzi katika madarasa ili kufikia idadi ya wanafunzi wasizidi 45 katika kila darasa na kuongeza ufaulu kwa kuleta matokeo mazuri kwa wanafunzi hao.

Akizungumzia mafanikio makubwa yanayoendelea kupatikana kwenye sekta ya elimu, Dk. Mwinyi alisema sekta hiyo imevuka malengo ya Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2021/ 2025 kwa kuboresha miundombinu ya kisasa.

Dk. Mwinyi alisema serikali itaajiri walimu wapya katika fani ya sayansi na hesabati ili kupunguza uhaba wa walimu sambambana maslahi ya walimu.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Khamis Abdalla Said alisema shule hiyo imejengwa na kampuni ya ujenzi wa Chuo cha Mafunzo Zanzibar (Magereza) na kusimamiwa na kitengo cha ujenzi cha Wizara ya Elimu na kugharimu Sh. bilioni 5.4 kutoka serikalini.

Aidha, alisema ujenzi wa shule hiyo umejumuisha madarasa 41, ofisi nne za walimu, ofisi ya mwalimu mkuu, vyoo 52, maktaba, maabara, chumba cha kompyuta na stoo na ukumbi mkubwa wa mikutano.

## Makamu wa Rais: Serikali inaendelea kuhamasisha uwekezaji

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Kwanza wa Rais Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema serikali ya Zanzibar inaendelea kuhamasisha uwekezaji endelevu wa miradi yenye tija na faida kubwa zaidi kwa wawekezaji, wananchi na taifa kwa jumla.

Aliyasema hayo jana visiwani Zanzibar kwa niaba ya Rais Dk. Hussein Mwinyi, alipomuwakilisha katika uzinduzi wa mpango wa Zanzibar wa uwekezaji unaozingatia malengo ya maendeleo endelevu sambamba na Dira ya Zanzibar ya Mpango wa Maendeleo ya Mwaka 2050.

Alisema hatua hiyo ni kuondokana na uwekezaji wa kuweka na kupata kiwango cha faida pekee bila kuangalia upande wa jamii, maendeleo ya nchi na utunzaji wa mazingira pamoja na matumizi ya ardhi, sambamba kiwango cha wenyeji wanavyoweza kufaidika na miradi inayowekezwa nchini.

Othman alisema mpango wa sasa uliozinduliwa unadhamira pia ya kuunganisha masuala yote muhimu ya maendeleo kwa nchi na jamii pamoja na wawekezaji ambao pia uwekezaji wenyewe utaepuka uharibufu wa mazingira. Alisema kwamba matunda ya uwekezaji kwa wananchi ni kufaidika vyema na uwekezaji uliopo kwa kuwa na uwezo bora na sahihi wa kuweza kuajiriwa katika uwekezaji uliopo au mwananchi mwenyewe aweze kuuhudumia uwekezaji huo kwa kuweza kupeleka bidhaa na huduma mbali mbali katika sekta husika.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Shariff Ali Sharif, alisema mpango huo unaozinduliwa unalenga jitihada makhususi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuhimiza uwekezaji endelevu katika maeneo makhusi ukiwemo uchumi wa buluu sambamba na kujenga imani kwa wekezaji kuja kuwekeza Zanzibar.

Aidha, alisema mpango huo pia utasaidia kuhamasisha Watanzania wanaoishi nje kuja kuwekezaza Zanzibar katokana na kuwepo sheria na taratibu bora za uwekezaji zinawahakikishia usalama wa fedha za pamoja na kuwepo wepesi wa usajili wa miradi kupitia TEHAMA

Mwakilishi mkaazi wa Shirika la Mpango wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa, Shegeki Komatsubara, alisema uzinduzi wa mpango huo umefanikiwa kutokana na juhudi za pamoja na ushirikiano kati ya shirika hilo na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ikilenga kuhamasisha mipango bora ya uwekezaji katika kusaidia kukuza uchumi na maendeleo ya Zanzibar.

## Wafanyabiashara wakamatwa na kilo 100 dawa za kulevya

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar imesema imekamata kilo 100 za dawa za kulevya aina ya methamphetamine, hashi na bangi katika operesheni waliyoifanya Januari mwaka huu.

Imesema dawa hizo ziliingizwa nchini na wafanyabiashara wakubwa ambao ni Salehe Khamis Basleman na Gawar Bachi Fakir wote wakazi wa Chukwani, Wilaya ya Magharibi Unguja.

Akizungumza na waandishi wa habari visiwani hapa, Kamishna Mkuu wa Mamlaka hiyo, Kanali Burhan Zubeir, alisema watuhumiwa hao wamekuwa wakifanya biashara hiyo Zanzibar, Tanzania Bara, Afrika, Asia, Ulaya na Marekani.

"Kupitia biashara hiyo wamejipatia kiasi kikubwa cha fedha ambazo wanazitumia kwa njia ya utakatishaji wa fedha haramu kwa kununua magari ya kifahari, nyumba, viwanja na kuanzisha biashara hewa" alisema.

Aidha, alisema fedha nyingine zinachepushwa kupitia akaunti mbalimbali za watu binafsi, wafanyabiashara na kampuni mbalimbali.

Alisema wahalifu wa aina hiyo wanatumia nguvu ya fedha na mbinu mbalimbali ili wasitambulike na waonekane watu wema katika jamii kwa kutoa misaada mbalimbali ikiwemo ujenzi na ukarabati wa nyumba za ibada, kuchimba visima vya maji, kufadhili mchezo wa mpira wa miguu na wengine wanahudumia watoto yatima.

Aidha, alisema serikali imedhamiria kwa dhati kudhibiti na kupambana na uhalifu wa dawa za kulevya Zanzibar bila kuangalia jina na wadhifa wa mtu.

Alisema kiasi hicho cha fedha ni kikubwa na kinaweza kuhudumia wizara mbili katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Alisema serikali itataifisha mali zote zilizotokana na uhalifu wa dawa za kulevya zilizopo ndani na nje ya Zanzibar kwa mujibu wa sheria.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA HATI YAKUSAFIRIA



**Veneranda Emmanuel Maswe,** Anatangaza kupotelewa kwa hati yake ya kusafiria (Passport) yenye namba **tae289055** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Dodoma tarehe 29/01/2020. Yeyote atakaeona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. TAARIFA YA POLISI: **PHQ/DOD/DOD/14296/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**KILATO STAPHODI EZEKIEL** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.3387/0052** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **MKONGORO SEKONDARI** mwaka 2017. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DOD/DOD/12322/2024.**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**Ndugu LYDIA SIMEO HENRY** anatangaza kupotelewa na kadi yake ya gari lenye namba za usajili **T 617 AQB.** Ametoa taarifa polisi na kupewa namba **PHQ/KAG/BUK/4469/2024,** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa polisi au apige simu namba **0754-757132.**

## KUPOTEA KWA KADI ZA GARI

**GUSTAV KRAMPE**

anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 167 AMZ.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote che polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DOD/DOD/9877/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI ZA MAGARI

**ALLY ZACHARIA RUKEZI** anatangaza kupotea kwa kadi za gari aina ya **PROBOX** zenye usajili namba **T 652 DFQ na T345 DJX,** CHASSIS NAMBA **NCPS10091454** na **NCPS10007406** na engine namba: **1NZR590407** na **1NZA521669.** Kwa yeyote atakaeziona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**PHQ/GEI/BUK/1887/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA TREKTA

**YOHANA HUMPHREY PETRO** anatangaza kupotelewa na kadi ya Trekta yenye namba za usajili **T 778 BJU** aina ya **MASSEY FERGUSON.** Chassis namba ***5008U42195.*** Engine namba IF31141U113963N. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote che polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/ARU/ARU/11662/2024.**

## TANGAZO LA KUPOTEA KWA HATI

**KWASLEMA BURA HHAWU** anatangaza kupotelewa na hati ya kiwanja chenye plot namba **20D block J.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/ARU/ARU/KAR/10967/2024.**

---

**FOMU MADAI - 3**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya TEMEKE**

**Kituo cha JUMUISHI Mkoa DAR ES SALAAM**

**Shauri la Madai/Ndoa Na. 579/2024**

**Jina la Mdai: MIQDAAD MOHAMEDALI RAMANI**

**Jina la Mdaiwa: SAYYADA NASIR JETHA**

**KUITWA SHAURINI**
**(Kanuni ya 18 ya Kanuni za Utaratibu wa Madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa: SAYYADA NASIR JETHA**

**Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/Wameleta madai yake/yao kwamba KUHUDHURIA MAHAKAMANI**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 29 Mwezi 04 Mwaka 2024 saa 3:30 asubuhi mbele ya Mhe. MLAPONI Hakimu Mkazi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinvyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama leo tarehe 18 Mwezi 04 mwaka 2024.

HAKIMU

---

**IN THE COURT OF DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**Probate and Administration Cause No 6649 of 2024**

**In the matter of the estate of the late CYPRIAN MNGOMA HAJI**

**And**

**In the matter of application for letters of administration by FRANK MATHEW HAJI**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules GN NO. 369 of 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letter of Administration is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on before the 20 day of MAY, 2024.

Dated at Dodoma this 23 day of April, 2024.

PETITIONER

PRINCIPAL / SENIOR / RESIDENT MAGISTRATE
DODOMA DISTRICT COURT

RESIDENT MAGISTRATE

---

**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA MJINI**

**Kituo cha CHAMWINO MJINI MKOA DODOMA**

**Shauri laMadai/Ndoa Na 57/2024**

**Jina la Mdai MAGUCHI MICROFINANCE COMPANY LIMITED**

**Jina la Mdaiwa IMAN ZAKAYO TWINOMUJUNI**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu Madai Katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa IMANI ZAKAYO**

**Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/ Wameleta madai yake/yao kwamba (Eleza hapa habari za Madai) TSH 3,500,000/=**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 18 Mwezi 04 Mwaka 2024 saa 2:00 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 05 Mwezi 04 Mwaka 2024

HAKIMU

---

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI. TUPIGIE: +255 - 0677 020701

AU

TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO, MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,

PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KITAIFA

## Kamati yashauri uwekezaji masoko ya hisa

**Na Vitus Audax,** DODOMA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria imewashauri Watanzania kuongeza uwekezaji katika masoko ya hisa na taasisi binafsi zenye tija na manufaa kwa taifa.

Mjumbe wa Kamati hiyo, Dk. Alice Kaijage, alisema hayo jana bungeni jijini hapa wakati akiwasilisha taarifa ya kamati hiyo kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji kwa mwaka 2023/24 pamoja na maoni ya kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya ofisi hiyo kwa mwaka 2024/25

Alisema serikali kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina ihakikishe inaweka makadirio ya makusanyo ya maduhuli yanayoakisi uwezo wa ukusanyaji wa hali halisi ya vyanzo vyake ili kuondoa hali ya baadhi ya miradi kutokupelekewa fedha kabisa za bajeti.

Pia alisema kamati inaitaka serikali kuongeza mitaji kwenye taasisi na mashirika ya umma, ili kuleta tija na kuongeza faida na kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara nchini, kwa kutoa huduma kwa wafanyabiashara na wawekezaji kwenye eneo maalum katika kila mkoa.

Vilevile, alisema ili kuondoa migogoro mbalimbali na wawekezaji, serikali itenge hifadhi ya ardhi kwa ajili ya uwekezaji pamoja na kutenga maeneo kwa ajili ya uwekezaji mahususi.

"Dira ya Mpango wa Maendeleo 2050 iendane na maendeleo ya nchi na watu sambamba na kufanya mabadiliko ya mifumo ya kiutawala hususani mifumo ya serikali za mitaa na kuhimiza matumizi ya mfumo wa kitaifa wa usimamizi wa miradi ya maendeleo (NPMIS) kwa watekelezaji wa miradi ya maendelelo," alisema.

Dk. Kaijage pia alisema kamati ilifanya uchumbuzi wa matumizi ya bajeti pamoja na upatikanaji wa fedha kwa mwaka 2023/24 na kubaini kuwa hadi kufikia Februari 2024, hakuna taasisi yoyote chini ya ofisi hiyo iliyopata kiasi cha fedha ambacho kinaendana na uwiano wa upatikanaji wa fedha kwa asilimia 66.6.

Alisema kwa ujumla, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, iliidhinishiwa Sh. bilioni 126.194 kwa mwaka wa fedha 2023/24 lakini hadi kufikia Februari, mwaka huu, ofisi ilipokea Sh. bilioni 57.663 pekee sawa na asilimia 46 ya bajeti iliyoidhinishiwa na Bunge.

Kamati hiyo iliishauri serikali fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ofisi hiyo zinapatikana kabla ya kumalizika kwa mwaka wa fedha 2023/24.

# RC agoma kukagua miradi aliyoandaliwa

**Na Francis Godwin,** IRINGA

MKUU wa mkoa wa Iringa Peter Serukamba, amekataa kuendelea na ziara ya kukagua miradi isiyo na changamoto aliyopangiwa na kutaka apelekwe kwenye miradi kiporo iliyokwama kutekelezwa kwa muda mrefu.

Mkuu huyo wa mkoa ambaye jana alipanga kuanza ziara yake katika Kata ya Ihemi na Ifunda alisitisha ziara yake majira ya saa 6 mchana baada ya kufika ofisi za Halmashauri ya Wilaya ya Iringa Vijijini mara baada ya kukabidhiwa taarifa ya miradi atakayokagua kwenye ziara hiyo.

Baada ya Kaimu Mkurugenzi kutambulisha watumishi waliokuwepo kwenye ukumbi huo wa halmashauri huku akimkaribisha msoma taarifa kusoma taarifa hiyo mbele ya mkuu huyo wa mkoa ghafla Serukamba alisimamisha zoezi hilo na kutaka kupewa idadi ya miradi yote inayotekelezwa katika halmashauri hiyo.

Hali iliyosababisha usomaji taarifa kusimama kwa dakika 10 wakati taarifa ya miradi hiyo ikifuatwa na baada ya kuletwa taarifa hiyo ya miradi alitaka kaimu mkurugenzi aoneshe miradi ambayo amepangiwa kukagua kama kwenye orodha ya miradi kiporo ya halmashauri hiyo ipo.

"Sasa hii miradi ambayo leo mnanipeleka ni miradi ipi kama kwenye orodha ya miradi yote kiporo ya halmashauri haipo mlitaka kuniingiza chaka wakati nilitoa maelekezo kuwa ziara yangu itaangazia miradi kiporo yote ambayo serikali ilikwisha toa pesa na haijakamilika," alisema Serukamba.

Alisema hawezi kuendelea na ziara ya ukaguzi wa miradi mizuri ambayo amepangiwa kwenye ratiba wala kwenda kufanya mkutano wa hadhara kijiji cha Ifunda kama hajatembelea miradi yote kiporo ambayo serikali ilikwisha toa fedha.

"Mimi sipo hivyo si kiongozi wa kukubali kudanganywa kirahisi hivi hii miradi mnayotaka kunipeleka ni miradi ambayo hakuna mafundi wanaoendelea na kazi nitakwenda kumuuliza nani huku na miradi mingi hapa mmenichagulia mizuri isiyo na dosari mimi nataka miradi yenye changamoto ili nijue shida ni nini na serikali ilikwisha toa pesa za kukamilisha miradi hiyo,"alisema.

Hata hivyo, aliagiza kusitishwa kwa ziara hiyo ili maofisa hao wa Halmashauri ya wilaya ya Iringa Vijijini kukaa kuchambua miradi yote kwa kanda ama tarafa au kata ili aweze kufika kukagua miradi hiyo na miradi ambayo watampeleka ni lazima wao wenyewe wawe walikwisha itembelea.

Hivi karibuni, kwenye kikao chake na watumishi wa halmashauri hiyo na madiwani baadhi ya madiwani walidokeza matumizi mabaya ya fedha za miradi kwenye halmashauri hiyo na kuwa miradi mingi imekwama kutokana na matumizi mabaya ya fedha.




Ofisa Mkuu Msimamizi wa Kodi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Lutufyo Mtafya (kulia), akitoa elimu kwa mfanyabiashara, Marik Nguti aliyefika katika banda la TRA wakati wa maonyesho ya makandarasi kwenye viwanja vya EPZ Bombambili, mkoani Geita jana, kwa lengo la kujifunza zaidi kuhusu kodi na kutoa ushuhuda wa namna elimu ya kodi ilivyomsaidia kuwabaini vishoka waliojitambulisha kama maofisa wa TRA waliotaka kuwatapeli wafanyabiashara wenzake. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Nchimbi ampigia waziri kukosekana soko la mahindi

**Na Halfani Chusi**

KATIBU Mkuu wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Balozi, Dk. Emmanuel Nchimbi amempigia simu Waziri wa Kilimo Hussein Bashe, kujibu

malalamiko ya wananchi wa Mbinga Mjini, mkoani Ruvuma ya kukosa soko la mahindi na kahawa.

Nchimbi alichukua uamuzi huo juzi alipotamatisha ziara yake ya kutembelea mikoa sita baada ya kulalamikiwa na mmoja wa wakulima kwa niaba ya wenzake kwamba mwaka jana walikosa soko la mahindi na wanahofu pia mwaka huu watakumbana na hali hiyo.

"Kuhusu suala la mahindi na mikopo kwa wakulima wa kahawa ngoja nimpigie Waziri wa Kilimo mumsikie wenyewe," aliwaambia wananchi hao.

Alipompigia waziri huyo alisema: "Ninadhani ulitoa maelekezo tulipofunga maghala ya Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA), kwamba tulipe madeni yaliyokuwa yamebaki kipindi cha nyuma na sasa

tunamalizia madeni yote, niwahakikishie wakulima wa Mbinga serikali itafungua tena maghala mengine na tutanunua mahindi yote kwa bei nzuri wasiwe na hofu.

"Mahindi yaliyobaki mwaka jana tutanunua na ya msimu huu mpya tutanunua kwa bei nzuri ruzuku ya mbolea itaendelea kutolewa kama ambavyo Rais Samia Suluhu Hassan ameelekeza, kwahiyo baada ya malipo hayo NFRA, itafungua maghala kuchukua mahindi ya mwaka jana na mwaka huu yaliyoko mikononi mwa wakulima," alisema Bashe.

Pia, alipiga marufuku tabia ya vyama vya ushirika kukopa fedha halafu jukumu la kulipa deni linabaki kwa wakulima akisistiza si haki.

Alitoa ufafanuzi wa gharama za magunia na kwamba mpango walionao baada ya bunge la bajeti watatangaza mfumo mpya wa ugharamiaji na uuzaji wa kahawa ambao utafanya iuzwe kweye vyama vya msingi baadaa ya

chama kikuu kujikusanyia na kufanya maamuzi.

Akikata simu ya Waziri Bashe Nchimbi aliwataka Watanzania kuwa na imani na CCM akiahidi kuendelea kuisimamia serikali kuhakikisha kero za wananchi zinatatuliwa kwa wakati.

Aliwaomba wafuasi hao kuhakikisha wanachagua wagombea waadilifu wanaoheshimu watu na walio tayari kutumikia wananchi ili waweze kujenga taifa kwa weledi.

Katibu wa Oganaizesheni Taifa, Issa Gavu aliwataka wananchi hao kujitokeza kwa wingi na kuwachagua viongozi wa chama hicho katika uchaguzi wa mwaka huu na mwakani.

Alisema hakuna viongozi wanaoweza kulileta taifa hili mafanikio nje na viongozi walioko ndani ya CCM, huku akiwasisitiza wananchi hao kufanya maamuzi sahihi muda wa uchaguzi utakapofika.

Katibu wa Itikadi Uenezi na Mafunzo Taifa, Amos Makalla, alisema lengo la ziara hiyo lilikuwa kuangalia uhai wa chama, utekelezaji wa ilani, maandalizi ya uchaguzi na utatuzi wa kero za wananchi.

"Mpaka kufikia leo tunahitimisha ziara yetu tuliyoifanya katika mikoa sita tumesikiliza na kutatua kero zaidi ya 100 kwanjia ya kisayansi (kimyakimya), lakini tumeridhishwa na namna mabalozi wa chama chetu

wanavyofanya kazi ya kuimarisha chama niwaombe tuendelee na moyo huo.

"Katika ziara hii tumejiridhisha kwamba CCM ni chama imara kutokana na namna Rais Samia anavyotatua kero za wananchi kila tulikopita tumepewa taarifa mabilioni ya shilingi yameingia kwaajili ya utekelezaji wa miradi mingi ikiwamo maji, umeme na afya.

Ziara hiyo ilianzia mkoa wa Katavi, Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na kutamatika Ruvuma.

# REFA WA DABI YA SIMBA, YANGA APELEKWA ZENJI

**Na Adam Fungamwango**

SHIRIKISHO la Soka la Zanzibar, (ZFF), limemtangaza mwamuzi Ahmed Arajiga, aliyechezesha mechi ya Simba na Yanga Jumamosi iliyopita kuwa mmoja wa marefa watakaochezesha michuano ya Kombe la Mapinduzi inayoanza leo visiwani Zanzibar.

Katibu Mkuu wa ZFF, Hussein Ahmada, alisema lengo la kumjumuisha mwamuzi huyo kutoka Tanzania Bara ni kuonyesha Muungano halisi, huku pia akisema wamechukua na watendaji wengine wa Shirikisho la Soka nchini (TFF), watakaoshirikiana na wenzao kuendesha michuano hiyo.

Mbali na Arajiga ambaye alichezesha dabi ya mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara na Yanga kushinda mabao 2-1, pia waamuzi wengine Amina Kyando na Frank Komba wameteuliwa kuchezesha michuano hiyo inayozishirikisha timu nne kutoka Bara na Visiwani, ambazo ni Simba na Azam, KMKM na KVZ.

„Kutoka Tanzania Bara tutakuwa na mwamuzi, Ahmed Aragija, Amina Kyando na Frank Komba, na wengine watatoka Zanzibar, hili ni Kombe la Muungano, tumewachukua na watendaji wengine wa TFF kuungana na wa ZFF kuendesha michuano hii ikiwa ni sura halisi ya Muungano,“ alisema katibu huyo.

Baadhi ya Watendaji walioteuliwa ni Mkurugenzi wa Ufundi wa TFF, Salum Madadi, Afisa Habari na Mawasiliano, Clifford Ndimbo na wengineo.

Ahmada, amebainisha kuwa msimu ujao kombe hilo litashirikisha timu nane badala ya nne zilizopo mwaka huu.

Akisema timu nne zitatoka Bara na nne Visiwani ili kuongeza mvuto na ushindani kwenye kombe hilo, ambalo linaanza leo.

Leo kwenye Uwanja wa New Amani Complex, KVZ FC itaikaribisha Simba Complex saa 2:15 usiku na kesho itakuwa zamu ya Azam FC kuvaana na KMKM SC uwanjani hapo na muda huo huo, ikiwa ni fainali ya pili. Washindi wa mechi hizo watakutana fainali uwanjani hapo, Jumamosi ijayo, Aprili 27, siku moja baada ya kilele cha Sikukuu ya Muungano.

**TUMEBEBA...**



Mchezaji wa mchezo wa Kuogelea wa Klabu ya Tallis, Raya Angemi, akipozi katika picha na makombe waliyotwaa kwenye mashindano Klabu ya Taifa ya Kuogelea yaliyomalizika mwishoni mwa wiki kwenye Bwawa Kuogelea la Shule ya Kimataifa Tanganyika (IST), iliyopo Masaki, Dar es Salaam. **PICHA: SHUFAA LYIMO**

# Kakolanya, Singida FG ngoma bado mbichi

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Singida Fountain Gate FC, umesema bado unatambua kipa Beno Kakolanya ni mali yao, lakini hatima yake itajulikana ndani ya saa 72 kuanzia jana.

Kupitia Ofisa Habari wa timu hiyo, Hussein Massanza, amesema suala la hatua gani itamchukulia kipa huyo ni baada ya Kamati ya Nidhamu itakapokutana na kujadili suala lake.

Kauli hiyo imekuja baada ya kipa huyo kugomea wito wa kamati hiyo ambayo ilitakiwa kukutana naye Aprili 19, mwaka huu, kwa ajili ya mahojiano na kumpa nafasi ya kujieleza.

Kipa huyo hakutokea katika kikao hicho na baadaye kuandika barua kwa kamati hiyo kuwa viongozi walifanya makosa ya kutoa tuhuma kuwa anaihujumu timu hiyo kwa kitendo cha kuondoka kambini kwa ruhusu ya Meneja wa timu.

Imeelezwa kipa huyo ameondolewa katika ‚group‘ (kundi) la mtandao wa kijamii la wachezaji ambalo anaweza kupata taarifa mbalimbali za klabu hiyo.

Akizungumza na Nipashe jana, Massanza alisema hatma ya kipa huyo adhabu au atasamehewa ni hadi kamati hiyo itakapokutana leo na ndani ya saa 72 watatoa maamuzi yao ila hadi sasa wanatambua Kakolanya bado ni mchezaji wao halali.

“Suala la kuondolewa katika group la timu na amekuja Mwanza kuchukuwa vitu vyake sifahamu, ninachafahamu ni kwamba kipa huyo hayupo kambini kabla ya kucheza mechi yetu dhidi ya Yanga, suala la adhabu gani atachukuliwa baada ya kugomea wito ni maamuzi ya kamati,” alisema Massanza.

Hata hivyo, chanzo chetu ndani ya klabu hiyo kilisema kipa huyo ameondolewa moja kwa moja ndani ya kikosi hicho baada kutuhumiwa kuwa anahujumu timu hiyo, hivi karibuni walipokuwa wakicheza na Yanga mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Alipotafutwa Kakolanya alieleza sababu ya kutokwenda kwenye kamati hiyo baada ya kupokea Barua ya wito wa Kamati ya Nidhamu Aprili 19, mwaka huu, aliipeleka kwa mwanasheria wake (hakumtaja jina), ambapo alimshauri wanapaswa kuwajibu kwanza,

“Mwanasheria wangu akaipitia vizuri Sana, baada ya hapo aliniambia lazima tuwajibu kwani kuna makosa Singida Fountain Gate FC wameyafanga kwa kutoa hukumu mitandaoni, kupitia ukurasa wao na kurasa zingine kubwa za mitandao ya kijamii.

„Kwa hiyo nikaandika barua ya kutokuhudhuria kwenye kikao cha kamati ya nidhamu kwa kuwa tayari wameshanihukumu hivyo hata nikienda kwenye kikao kitakuwa si halali na ni kinyume cha sheria. Wao walitakiwa waniite kwanza wanisikilize kabla ya kutoa hukumu kwa hiyo kwenye kikao hicho nisingepata haki yangu ya msingi,” alisema Kipa huyo.

## Kurugenzi yapata ushindi wa chee kutoka kwa Dar City

**Na Adam Fungamwango**

BODI ya Ligi imeipa ushindi wa wa mabao matatu Kurugenzi FC, baada Dar City kubainika kuchezesha wachezaji wawili ambao walitumia leseni za kughushi katika mechi ya Ligi Daraja la Pili, ‚First League‘, uliochezwa Aprili 6, mwaka huu, kwenye Uwanja wa Kambarage, Shinyanga, na timu hizo kutoka suluhu.

Uamuzi huo umetolewa na Kamati ya Uendeshaji na Usimamizi wa Ligi ya Bodi ya Ligi Kuu Tanzania (TPLB), iliyokaa Aprili 16, mwaka huu huku walipobainika kufanikisha vitendo hivyo wakipewa adhabu pia.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Idara ya Habari na Mawasiliano ya Bodi ya Ligi, Dar City iliwatumia wachezaji, Mohamed Ismail na Herman Beatus Damas, ambao walitumia leseni za kughushi katika mechi hiyo ya kwanza ya ‚play off‘ iliyochezwa siku hiyo.

„Klabu ya Dar City imepoteza mchezo huo na kutozwa faini ya Sh. 300,000 huku wachezaji hao wakifungiwa kucheza soka kwa miezi 12, kwa mujibu wa kanuni ya 48:23 ya First League, kuhusu udhibiti wa klabu.

„Kocha Mkuu wa Dar City, Almasi Shaaban, amefungiwa kwa kipindi cha mwaka mmoja na kutozwa faini ya Sh. 500,000 kwa kosa la kuwachezesha wachezaji ambao alifahamu fika ni batili,“ ilisema taarifa hiyo.

Aidha, Katibu wa klabu hiyo, Ephraim Augustine pia amekutana na nyundo na kufungiwa mwaka mmoja na kutozwa fainali ya Sh 500,000 kwa kosa la kutoa nyaraka za udanganyifu ambazo ni leseni za wachezaji hao na kuziwasilisha kwa maafisa wa mchezo huo kwa lengo ovu la kufanikisha wachezaji hao batili kutumika katika mchezo huo.

Ilikuwa ni mechi ya ‚play off‘ ambapo timu hizo zilikuwa zinagombania kubaki kwenye kwenye ligi hiyo, baada ya kufanya vibaya na kujikuta zipo kwenye nafasi hiyo.

Wakati huo huyo, timu ya KenGold ambayo tayari imepanda daraja na kutarajia kucheza Ligi Kuu msimu ujao, imetozwa faini ya Sh. 1,500,000 kwa kosa la kukataa kutumia chumba maalum cha kuvalia kilichoandaliwa kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, Arusha katika mchezaji wake dhidi ya TMA, ambao ilishinda bao 1-0, Aprili 13, mwaka huu.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### ZEBRI AWANIWA UNITED
KOCHA wa Brighton, Roberto de Zerbi, ndiye mgombea anayeongoza kuchukua nafasi ya Erik Ten Hag ikiwa ataondoka Old Trafford, na Seagulls wanamfikiria kocha mkuu wa Burnley, Vincent Company kama mbadala wake. (***Teamtalk***)

### AMORIM ATAJWA WEST HAM
KLABU ya West Ham itafanya mazungumzo na kocha mkuu wa Sporting Lisbon, Ruben Amorim, mwenye umri wa miaka 39, huku bado wakiwa hawajaamua iwapo wataongeza mkataba wa David Moyes msimu huu wa majira ya joto. (***The Athletic***)

### MOYES KWENYE RADA
KOCHA wa zamani wa Wolves, Julen Lopetegui, ni mshindani mkubwa kuchukua nafasi ya David Moyes katika Klabu ya West Ham. (***Telegraph***)

### LIVER YAKOMAA NA AMORIM
RUBEN Amorim anasalia kuwa chaguo la kwanza la Liverpool kuchukua nafasi ya Jurgen Klopp, lakini kocha wa Brentford, Thomas Frank anazingatiwa ikiwa Mreno huyo ataenda kwingine. (***Team Talk***)

### TEN HANG KUTATHMINIWA
UWEZEKANO wa Erik ten Hag utatathminiwa na Mkurugenzi mpya wa Ufundi wa Manchester United, Jason Wilcox, kabla ya klabu hiyo kufanya uamuzi kuhusu mustakabali wa Mholanzi huyo. (***Telegraph***)

### BRUYNE BADO AWINDWA
KLABU Al-Nassr ya Saudi Arabia bado ina nia ya kumsajili Kevin de Bruyne wa Manchester City msimu wa majira ya joto na inatarajiwa kuwasiliana na kiungo huyo wa kati wa Ubelgiji mwenye umri wa miaka 32 hivi karibuni. (Rudy Galetti)

### BARCA, ARSENAL KWA ISAK
BARCELONA imeiungana na Arsenal kutaka kumnunua mshambuliaji wa Newcastle United na Sweden, Alexander Isak mwenye umri wa miaka 24, ambaye thamani yake inatajwa kuwa ni pauni milioni 90. (***Sun***)

### OLISE AGEUKA LULU
ARSENAL na Manchester United zimeingia kwenye kinyang'anyiro cha kumsajili winga wa Crystal Palace na Ufaransa, Michael Olise mwenye umri wa miaka 22, lakini wanakabiliwa na ushindani kutoka kwa Chelsea, Manchester City na Juventus. (***Football Insider***)

### GYOKERES KUONGEZA WATATU
ARSENAL inatarajia kuongeza wachezaji watatu au wanne msimu huu wa majira ya joto huku wakikamilisha kufanyia marekebisho kikosi chao, na tayari mshambuliaji wa Sporting Lisbon na Sweden, Viktor Gyokeres mwenye umri wa miaka 25, akiwa lengo lao kuu. (***Footbal Transfer***)

### BRANTHWAITE ALENGWA
KLABU ya Manchester United imemfanya beki wa Everton na England mwenye umri wa miaka 21, Jarrad Branthwaite, kuwa shabaha yao kuu msimu huu. (***Football Insider***)

### DE GEA ATAKIWA BETIS
REAL Betis inalenga kumsajili mlinda mlango wa zamani wa Manchester United na Hispania, David de Gea mwenye umri wa miaka 33, ambaye amekuwa mchezaji huru tangu kuondoka Old Trafford mwishoni mwa msimu uliopita. (***Estadio Deportivo***)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MOURINHO: MAN UTD BADO INA WACHEZAJI AMBAO SIKUWATAKA

**LONDON, England**

KOCHA wa zamani wa Manchester United, Jose Mourinho, amesema klabu hiyo bado ina wachezaji ambao hakuwapenda kwenye kikosi hicho wakati alipokuwa kocha.

**Kocha huyo raia wa Ureno, alijiunga na Man United msimu wa majira ya joto wa 2016 na aliiongoza klabu hiyo katika michezo 144 katika mashindano yote kabla ya kupoteza kibarua chake mwaka 2018 baada ya matokeo mabaya, akiwa ameshinda Ngao ya Jamii, Kombe la EFL na Ligi ya Europa pale Old Trafford.**

Sasa akiwa hana timu baada ya kutimuliwa AS Roma, Mourinho amefunguka kuhusu uhusiano wake na Mtendaji Mkuu wa zamani wa Man United, Ed Woodward, na kudokeza kuwa angefanya mabadiliko kwenye kikosi cha sasa.

> ●●● Ningependa Manchester United ifanikiwe, na hao si wasifu bora zaidi kwa mwelekeo wa...

Katika mahojiano na The Telegraph, alisema: „Sikuwa na kiwango hicho cha uaminifu ambacho Erik ten Hag anacho. Kwa hiyo niliondoka kwa huzuni, kwa sababu nilihisi nilikuwa mwanzoni mwa mchakato.

„Wakati fulani, nilihisi kama wananiamini na kuamini uzoefu wangu, lakini mambo yalikuwa tofauti.

"Bado kuna wachezaji kadhaa ambao sikuwataka miaka mitano au sita iliyopita. Nadhani wanawakilisha kidogo. Ninaona kuwa si wasifu bora zaidi wa kitaaluma kwa klabu ya mwelekeo fulani.

„Lakini nilifanya kazi yangu huko. Muda unasema ukweli kila mara. Ningependa Manchester United ifanikiwe."

Mourinho aliwanunua nyota wa hadhi ya juu kama Paul Pogba, Zlatan Ibrahimovic na Romelu Lukaku wakati akiwa kocha wa Man Utd, huku wachezaji wa sasa wa kikosi cha kwanza, Marcus Rashford na Anthony Martial alikuwa akiwatumia mara kwa mara pale Old Trafford.

Bosi huyo wa zamani wa Chelsea pia alikuwa na uhusiano mbaya na beki wa kushoto, Luke Shaw.



# TUCHEL ATAKA KURUDI TENA EPL

**MUNICH,** Ujerumani

KOCHA wa Bayern Munich, Thomas Tuchel, nia yake kubwa kwa sasa ni kurejea kwenye Ligi Kuu England, EPL, licha ya kutakiwa na Barcelona, kwa mujibu wa ESPN.

Tuchel anatazamiwa kuondoka Bayern mwishoni mwa msimu huu, licha ya kuwaongoza kutinga nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Chanzo kimoja kimeiambia ESPN kwamba Barcelona wamemfanya kocha huyo mwenye umri wa miaka 50, kuwa mgombea wa kuchukua nafasi ya Xavi Hernandez, ambaye pia anatarajiwa kuachia wadhifa wake msimu huu wamajira ya joto.

Lakini Tuchel, ambaye aliiongoza Chelsea kati ya Januari 2021 na Septemba 2022, angependelea kupata kazi nchini England.

Kocha huyo wa zamani wa Borussia Dortmund na Paris Saint-Germain hajakataa kujiunga na Barcelona ikiwa wanataka kumpa ofa, lakini chanzo kiliiambia ESPN kwamba ana wasiwasi kuhusu uthabiti wa klabu hiyo, haswa jinsi ukosefu wa fedha za uhamisho unaweza kukwamisha mipango ya kuimarisha kikosi.

Mchezaji wa zamani wa Timu ya Taifa ya Mexico, Rafael Marquez na kocha wa zamani wa Ujerumani, Hansi Flick pia wanawaniwa na Barcelona.

Tuchel atakuwa tayari kuzungumza na Manchester United ikiwa nafasi itafunguliwa.

Kocha wa sasa wa United, Erik ten Hag, yuko katika shinikizo pale Old Trafford baada ya msimu wa pili wa kuinoa timu hiyo ambayo haijawa na matokeo mazuri sana pamoja na kuwasili kwa mmiliki mwenza mpya, Sir Jim Ratcliffe.

Vyanzo vya klabu vimeiambia ESPN kuwa bado hawajafanya uamuzi juu ya hatma ya Ten Hag na kwamba kuna uungwaji mkono ndani ya timu ya Ratcliffe kwa Tuchel ikiwa Mholanzi huyo ataondoka na wawakilishi wametakiwa kufahamishwa kuhusu mustakabali wa Mjerumani huyo.

Tuchel, ambaye alishinda Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na Chelsea mwaka wa 2021, amefurahia mafanikio katika kinyang'anyiro hicho akiwa na Bayern msimu huu huku timu yake ikipangwa kukutana na Real Madrid katika nusu fainali.

Hata hivyo, amesimamia kampeni mbaya ya ndani, akisalimisha taji la Ujerumani kwa mara ya kwanza tangu 2012 na kupoteza katika raundi ya pili ya Kombe la Ujerumani.

Ilitangazwa Februari kwamba Tuchel ataondoka Bayern mwishoni mwa msimu.

Juhudi za kumshawishi Julian Nagelsmann kujiunga tena na klabu hiyo zimeambulia patupu baada ya kocha huyo mwenye umri wa miaka 36, kutia saini mkataba mpya wa kusalia kuinoa Timu ya Taifa ya Ujerumani hadi 2026.

## Araujo atamani kubaki Barcelona




**BARCELONA,** Hispania

RONALD Araujo amezungumzia kuhusu nia yake ya kusalia Barcelona licha ya ripoti kudai kuwa klabu hiyo inaweza kumuuza.

Ili kukabiliana na matatizo yao ya kifedha yanayoendelea, Barca wanaweza kulazimika kufanya mauzo makubwa wakati wa dirisha la uhamisho wa majira ya joto, na Araujo anaonekana kuwa mmoja wao.

Manchester United, Bayern Munich na Atletico Madrid zote zimehusishwa na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, ambaye anaweza kuleta euro milioni 100 kwa klabu ikiwa mauzo yatafanywa.

Lakini Araujo amebainisha nia yake ya kubaki Barcelona na fahari yake ya kuchezea jezi za rangi za klabu hiyo.

Akizungumza na Diario AS, kuhusu uwezekano wa mazungumzo ya mkataba mpya raia huyo wa Uruguay alisema: „Ukweli ni kwamba yanaendelea vizuri. Klabu imeanza mazungumzo na mawakala wangu. Tunafikiria kuhusu michezo hii na kile kilichosalia cha msimu. Na msimu utakapofika mwisho watakaa chini na kuzungumza.

„Siku zote huzungumzwa juu ya siku zijazo na mapendekezo. Kila mwaka itakuwa hivi, lakini nina furaha Barcelona, familia yangu ina furaha. Ninapotoka natoa kila kitu na nataka Barca iwe Barca ya zamani, nitaipigania hadi kufa kwa jezi hii."

## Arteta: Chelsea itafanikiwa chini ya kocha Pochettino

**LONDON,** England

MIKEL Arteta amesema Chelsea itapata mafanikio chini ya Mauricio Pochettino kwa sababu matumizi makubwa ya fedha bado ni njia kuu ya mafanikio kwenye Ligi Kuu England.

Arsenal waliwakaribisha wapinzani wao hao wa London katika Uwanja wa Emirates jana Jumanne wakilenga kusogea mbele kwa pointi nne dhidi ya Manchester City kileleni mwa Ligi Kuu.

Chelsea itamaliza msimu wa kwanza wa Pochettino bila taji na wanakabiliwa na uwezekano wa kutofuzu kucheza Ulaya ikizingatiwa kuwa wako katika nafasi ya tisa baada ya kufungwa mara 10 kwenye ligi msimu huu.

Chelsea wametumia zaidi ya pauni bilioni moja tangu kuchukuliwa na Todd Boehly alipokamilisha ununuzi Mei 2022 na alipoulizwa Jumatatu kama anahisi Chelsea itaimarika, Arteta alisema: „Nina hakika watafanya hivyo. Kwa kikosi hicho, ndio, na kwani kocha wanaye.

"Ukiangalia historia ya Ligi Kuu kwa miaka 20 iliyopita kwenye zile ambazo zimetumia fedha nyingi na kilichotokea kuna uhusiano mkubwa.

„Wanastahili kuwa katika nafasi ya juu zaidi kwenye ligi ukiangalia wamefanya nini na wanachozalisha kwenye michezo. Wamefika fainali ya Carabao, wametinga nusu fainali ya Kombe la FA.

„Nadhani anachofanya Mauricio ni cha kuvutia sana na nina uhakika atawafikisha huko."



HABARI MICHEZO

# MREFA, SOREFA ZAIPONGEZA KENGOLD KUPANDA LIGI KUU

Na Adam Fungamwango

CHAMA cha Soka Mkoa wa Mbeya (MREFA) na cha Wilaya ya Songwe (SOREFA), zimeipongeza Klabu ya KenGold kwa kufanikiwa kupanda daraja, ambapo sasa itacheza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2024/25, vikisema ni heshima kubwa kwa mkoa huo ambao umekuwa na rekodi ya kupandisha timu mara kwa mara.

Mwenyekiti wa MREFA, Sadick Jumbe, amesema anawapongeza wachezaji na viongozi wa timu hiyo, akiwataka sasa kukiimarisha kikosi kwa ajili ya kukabiliana na mikiki ya Ligi Kuu msimu ujao.

Jumbe, alisema haikuwa bahati mbaya kwa KenGold kupanda kwani ni mikakati iliyofanywa na klabu hiyo pamoja na wao kama chama cha soka, huku akifichua lengo lilikuwa ni kupandisha timu mbili kati ya tatu zilizokuwa zikicheza Ligi ya Championship.

„Lengo letu la kwanza lilikuwa ni kuingiza timu mbili kati ya tatu zilizokuwa Championship, ambazo ni KenGold, Mbeya City na Mbeya Kwanza zipande Ligi Kuu.

Bahati mbaya sana, Mbeya City imeshajiondoa, lakini Mbeya Kwanza bado inapigana, inaweza kupata nafasi ya kupanda kwenye mechi za mchujo, bado hatujakata tamaa," alisema Jumbe.

Naye Mwenyekiti wa SOREFA, Jocob Mwangosi, alisema anaungana na Wanambeya wote kushehekea kupanda kwa timu hiyo, huku Afisa Michezo wa Mbeya, Robert Mfugale, akibainisha kuwa safari ya timu hiyo haikuanza leo bali ni ya misimu mitatu nyuma, ambapo ilikuwa ikihangaika kutaka kupanda, lakini haikukata tamaa ikaendelea kupambana na leo inakula matunda ya uvumilivu.

Ijumaa iliyopita kwenye Uwanja wa Kumbukumbu ya Sokoine jijini Mbeya, timu hiyo ilifanikiwa kupanda Ligi Kuu baada ya kuifunga FGA mabao 2-0 yaliyoifanya kufikisha pointi 67, ambazo zinaweza kufikiwa na timu moja tu ya Pamba FC, huku timu zote zikisaliwa na mechi moja.

## Mbisa arejea uwanjani baada ya msimu mmoja

Na Adam Fungamwango

GOLIKIPA wa timu ya Prisons, Mussa Mbisa, juzi alicheza mechi yake ya kwanza akiwa na timu hiyo msimu huu tangu alipoumia Ligi Kuu Tanzania Bara msimu uliopita.

Akizungumza baada ya kurejea uwanjani, alisema anashukuru kuwa amekaa langoni baada ya muda mrefu na hakuruhusu bao katika mechi ambayo timu yake ilitoka suluhu dhidi ya Kagera Sugar, mechi ikichezwa Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya.

„Nashukuru nimerejea, nimekaa langoni baada ya muda mrefu na sijaruhusu bao, kikubwa kilichobaki ni kuwa na mwendelezo mzuri, kufanya vema katika michezo itakayokuja mbele kila nitakapopewa nafasi kwa sababu hapa Prisons, magolikipa wote sisi watatu ni wazuri, kila mmoja ana kitu chake kimoja ambacho anawashinda wenzake, kikubwa kila anayepewa nafasi aitendee haki kwa sababu nyuma kuna wengine.

„Kwangu mimi niliona kama kocha amenipa deni kubwa, nimetoka kwenye majeraha, lakini amenipa namba, nimekaa langoni kwa uangalifu mkubwa ili nisije nikamvunja moyo kocha wangu, Ahmad Ally, aliyeniamini," alisema Mbisa ambaye amewahi kuzidakia Klabu za Mwadui na Coastal Union.

Kipa huyo aliumia katika mchezo wa Ligi Kuu msimu uliopita katika mechi ambayo timu yake ilicheza dhidi ya Singida Big Stars na kulazimika kutolewa nje na kukimbizwa hospitali, tangu hapo alikuwa akiuguza jereha la mguu.

Katika mechi yake ya kwanza ambayo ametoka na 'clean sheet', ameisaidia timu yake kupata pointi moja na kufikisha 31, ikiwa nafasi ya sita kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, huku timu iliyocheza nayo, Kagera Sugar ikiwa nyuma yake nafasi ya saba, ikikusanya pointi 29.



KAZINI LEO...



Wachezaji wa Simba wakiwasili Zanzibar jana tayari kwa michuano ya Kombe la Muungano, ambapo leo itashuka katika Uwanja wa New Amaaan Complex kuvaana na KVZ FC kwenye mchezo wa nusu fainali. **MPIGAPICHA WETU**

## Benchikha bado...

INATOKA UK. 24

kufanya vizuri katika mchezo wa kwanza wa nusu fainali dhidi ya KVZ FC ya visiwani humo. Simba leo saa 2:15 usiku inamenyana na wenyeji, KVZ katika Nusu fainali ya Kombe la Muungano, itakayopigwa Uwanja wa New Amaan Complex visiwani, Zanzibar wakati Azam FC Alhamisi itavaava na KMKM, na Washindi wa mechi za hizo za watakutana katika fainali ya michuano hiyo Aprili 27, mwaka huu uwanjani hapo.

## Mvua yazuia mechi Yanga, JKT Tanzania

INATOKA UK. 24

kuangalia mazingira ilijiridhisha kuwa inaweza kuchezwa, kabla ya mvua kunyesha tena mchana na kuongeza ubovu wa miundominu kwenye uwanja huo.

Kuahirishwa kwa mechi hiyo kunafanya timu zote tatu za juu, Yanga, Azam na Simba kutocheza mechi zao wiki hii.

Simba na Azam zipo Zanzibar kucheza michuano ya Kombe la Muungano, ambalo Yanga ilijitoa kwa kile ilichodai ni kubanwa kwa ratiba ya mashindano yake, mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara, pamoja na Kombe la FA.

# Michezo

Jumatano Aprili 24, 2024

Nipashe


UK. 22



Arteta amtabiria makubwa Pochettino Chelsea

# Benchikha bado yupo sana Simba

## ●●● Uongozi wasema tayari umekutana naye kwa mkakati wa msimu ujao, hivyo...

**Na Saada Akida**

WAKATI leo akikiongoza kikosi chake kuivaa KVZ FC kwenye mechi ya Kombe la Muungano, Klabu ya Simba imesema haina mpango wowote wa kuachana na kocha wao, Abdelhak Benchikha, kama inavyoanza kuvumishwa na baadhi ya watu, huku ikiweka wazi kuwa tayari imeshakutana naye kwa ajili ya kujadili tathimini ya maboresho ya kikosi cha timu hiyo kwa msimu ujao wa mashindano.

**Kauli hiyo inakuja baada ya kuwapo kwa taarifa katika mitandao mbalimbali na baadhi ya wachambuzi wa soka juu ya kocha huyo, wakidai yupo hatarini kutupiwa virago kuondoka ndani ya timu hiyo baada ya matokeo mabovu.**

Akizungumza na Nipashe jana, Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema hakuna ukweli juu ya nia yoyote au mpango wa kumtimua au kusitisha mkataba na Benchikha kwani ni kocha mkubwa Afrika na wanamuamini.

Aliwataka mashabiki kutulia kwa kipindi hiki cha mpito na kuimarisha nguvu na mshikamano kwa ajili ya kuimarisha timu yao kwa msimu ujao kulingana na mapendekezo ya benchi la ufundi linaloongozwa na Benchikha.

“Hatuna mpango huo wa kumuondoa au kuachana na Benchikha, Wanasimba wanatakiwa kupuuza taarifa zilizosambaa kuhusu kocha wetu, bado yupo kwenye mipango ya klabu na sasa wazo na mikakati yetu ni kuboresha na kujenga timu ya msimu ujao, lakini pia kuhakikisha tunafanya vizuri katika michezo iliyopo mbele yetu.

„Benchikha yupo sana na leo (jana) mchana alikuwa sehemu ya timu iliyoenda visiwani Zanzibar kwa ajili ya michuano ya Kombe la Muungano ikiwa ni sehemu ya mipango ya kuhakikisha tunafanikiwa kushinda kombe hilo,” alisema Ahmed.

Aliongeza kuwa kikosi kipo vizuri na wachezaji wote wako salama na wako kwenye msafara huo kasoro wawili, beki Shamari Kapombe, aliyeumia kwenye mazoezi ya kujianda na michezo ya Kombe la Muungano.

Ahmed alisema mchezaji mwingine ambaye hajaambatana na timu ni kiungo Sadio Kanoute mwenye majeraha baada ya kuumia kwenye mchezo wa dhidi ya Yanga wikiendi iliyopita.

Alisema wachezaji wapo tayari kwa ajili ya michuano hiyo ya Kombe la Muungano kwa

INAENDELEA UK. 23



Benchikha

# Mvua yazuia mechi Yanga, JKT Tanzania

**Na Adam Fungamwango**

MVUA kubwa inayoendelea kunyesha, Dar es Salaam, imesababisha mechi ya Ligi Kuu namba 125 kati ya JKT Tanzania iliyokuwa mwenyeji wa Mabingwa Watetezi, Yanga, iliyokuwa ichezwe jana jioni kuahirishwa kutokana na baadhi ya sehemu ya Uwanja wa Meja Jenerali, Isamuhyo uliopo Mbweni nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam kujaa maji.

Akitangaza kuahirishwa mechi hiyo, Kamisaa wa mchezo huo, Kamwanga Tambwe, alisema mechi hiyo imeahirishwa baada ya kujiridhisha kuwa uwanja hauko katika hali nzuri ya kuweza kuruhusu mchezo huo kupigwa kikanuni.

Alisema kutokana na hali ya uwanja kuwa mbaya, kwa kushauriana na wenzake wameamua kuahirisha mchezo huo, na taarifa zitapelekwa Shirikisho la Sona nchini (TFF) na Bodi ya Ligi kwa maamuzi zaidi.

"Kanuni zinasema mechi ikiahirishwa kama hivi inaweza kurudiwa kesho (leo), au siku nyingine itakayopangwa, lakini kama ulikuwa umechezwa hata kwa sekunde moja, au zaidi, basi ilikuwa ni lazima mchezo urudiwe kesho, kwa maana hiyo, tunapeleka taarifa juu, huko wao ndio wataamua kwa mujibu wa kanuni zikavyoyoelekea, lakini sisi tumejiridhisha kuwa mchezo hauwezi kuchezwa.

Timu zote mbili zilikuwa zimefika uwanjani zikifanya mazoezi ya mwisho kabla ya mchezo huo, lakini kilichokuwa kinaonekana ni eneo la katikati ya uwanja ndilo lililokuwa na maji yaliyotuama, huku maeneo mengine yalionekana kuwa yako vizuri.

Mechi hiyo inaingia katika rekodi ya kuwa ya kwanza kuahirishwa kwa sababu ya sababu za akiasili msimu huu.

Awali, kuliwa na tetesi za mchezo huo kuahirishwa mapema asubuhi, lakini Bodi ya Ligi baada ya

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >